Nipashe
Jumamosi Februari 8, 2025 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581946 www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0677 020 710 LIKE & FOLLOW US Nipashe digital
epaper.ippmedia.com MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii www.ippmedia.com

UKURASA WA 3 & 17
**Wakuu** SADC, EAC kujifungia Dar, hali yazidi kuwa mbaya DRC

UKURASA WA 3
**Vigogo** matatani madai kuchepusha majisafi na salama mashambani mwao

UKURASA WA 5
**RPC** aagiza waliotafuna fedha za soko wakamatwe



**VAN DIJK: TUMESHINDA, ILA HATUKUCHEZA VIZURI** UKURASA 22

# Makali hatua za Trump yaanza kung'ata rasmi

• **Watumiaji** ARV sasa kununua ... *Endelea Ukurasa 2*



Rais wa Marekani, Donald Trump

Waziri wa Afya, Jenista Mhagama

RIPOTI MAALUM:

# Wazazi wacharuka wanafunzi wa darasa la IV kusoma hadi usiku

• **Walimu** watoa sababu, serikali yaweka msimamo... *Uk. 4*

## Mikopo ya asilimia 10 halmashauri kaa la moto

UKURASA 2

**MICHEZO** **FADLU AMKINGIA 'KIFUA' CHASAMBI** UK.24

**MAONI,** UK.6

## Fedha za mikopo halmashauri kaa la moto

**Augusta Njoji na Jenifer Gilla**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, amesema fedha za mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ni za 'moto' na kiongozi wa mkoa, wilaya na halmashauri atakayebainika eneo lake kuwa na kikundi hewa atawajibishwa.

Akizungumza jana kwenye hafla ya utiaji saini mikataba ya utoaji mikopo hiyo kati ya halmashauri 10 na benki tatu jijini Dodoma, Mchengerwa alisema: "Kabla ya Waziri hatawajibika, atawajibika mkuu wa mkoa, Wilaya na Wakurugenzi nawaambia wazi kabisa, tumefika hapa kwasababu kuna watumishi wasio waaminifu ambao walitafuna fedha hizi kwa kukopeshana wenyewe na hawakuwa na sifa ya kupokea mikopo hii."

Mchengerwa alisema kila mmoja afuatilie fedha hizo na hatarajii kusikia vikundi hewa na kusisitiza zikishuka kama ilivyokusudiwa kwa walengwa ili zitabadili maisha yao.

Alisisitiza uadilifu wa kwenye fedha hizo na kufuatilia kwa kina vikundi vyote na kuvijua na asisikie vikundi hewa.

"Fedha hizi ni za moto. Wajibu wetu ni kumsaidia Rais zisiende kuchezewa. Naelekeza kikundi hewa kitakachobainika eneo lolote viongozi wa eneo hilo mtapaswa kuwajibika, tumieni vyombo mnavyosimamia kwenye mikoa na wilaya kuhakikisha hakuna vikundi hewa, fedha zisimamiwe na kurejeshwa," alisema.

Alisema kanuni zimeboreshwa zinawapa nguvu maofisa maendeleo ya jamii na benki zinazotoa fedha hizo kufuatilia, kusimamia na kuvikagua vikundi kabla ya kutoa fedha hizo.

"Nazielekeza mamlaka za serikali za mitaa kuendelea kuchangia fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya mikopo hii kwa mujibu wa sheria ya fedha za serikali za mitaa, na Katibu Mkuu niletee orodha kama kuna halmashauri ambazo hazijachangia na zinadorora kuchangia na kama kuna halmashauri ambayo haijatekeleza ya maelekezo ya Rais," alisema.

Waziri Mchengerwa alisema vikundi vyote vinavyopokea mikopo hiyo vinatakiwa kufanya shughuli za uzalishaji na kurejesha fedha kulingana na mipango ya marejesho.

"Wakuu wa mikoa, wilaya na wakurugenzi tumekubaliana jukumu la usimamizi wa fedha hizi ni la kila mmoja wetu na wakati tunamshauri Rais sisi wizara tulimhakikishia kuanzia kwangu kwamba iwapo kutakuwa na kulegalega kukote mimi na wasaidizi wangu tutalazimika kuwajibika," alisisitiza.

Alisema benki ya NMB itafanya kazi kwenye halmashauri za wilaya za Bumbuli, Itilima, Newala, Manispaa ya Songea, Jiji la Dodoma huku benki ya CRDB itafanya kazi wilaya za Nkasi, Mji wa Mbulu, Manispaa ya Kigoma na Jiji la Dar es Salaam huku Benki ya Biashara ya Uchumi ikifanya katika Halmashauri ya Wilaya ya Siha.

Zaidi ya Sh. bilioni 234 zinakusudiwa kupelekwa kwa wananchi kwa njia mbili za utoaji mikopo hiyo ambazo ni kupitia benki kwa halmashauri 10 na mikopo iliyoboreshwa kwenye halmashauri 174.

Mikopo hiyo, alisema inatarajiwa kunyanyua uchumi wa taifa na wa mtu mmoja mmoja kupitia vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Naye Katibu Mkuu wa TAMISEMI, Adolf Ndunguru, alisema kutiwa saini mikataba hiyo ni mwanzo wa mapinduzi ya kuhakikisha mikopo hiyo 10 inakuwa na tija tofauti na ilivyokuwa miaka ya nyuma huku Meya wa Jiji la Dodoma, Prof. Davis Mwamfupe, akisema licha ya mfumo wa taarifa za wakopaji kuwa kidijitali ni vyema mikopo hiyo kuangaliwa inafanya kazi gani.



Rais wa Zanzibar, Alhajj Dk. Hussein Ali Mwinyi, akitia saini kitabu cha maombolezi kufuatia kifo cha Kiongozi Mkuu wa 49 wa Madhehebu ya Shia Ismailia Duniani na Mwanzilishi wa Mtandao wa Maendeleo wa Aga Khan (AKDN), Prince Karim Al -Hussaini Aga Khan IV, aliyefariki dunia Jumanne wiki hii, jijini Lisbon Ureno, alipofika katika Jamaat la Shia Ismailia Zanzibar Hurumzi, Wilaya ya Mjini Unguja jana. Kushoto ni Mkuu wa Jamaat la Shia Ismailia Zanzibar, Altaf Jiwan. **PICHA: IKULU**

# Makali hatua za Trump yaanza kung'ata

**Na Restuta James**

WANAOISHI na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (VVU) wamedai kwamba katika maeneo wanakochukulia dawa wameambiwa dozi za kufumbaza virusi (ARV) zitaanza kuuzwa (bei inahifadhiwa).

Hatua hiyo inatokana na uamuzi uliotangazwa hivi karibuni na Rais wa Marekani, Donald Trump, kuhusu mabadiliko ya Sera ya Mambo ya Nje ya nchi hiyo.

Kutokana na mabadiliko hayo, athari zingine wanazotaja ni kwa wajawazito na wanaonyonyesha, wanaotumia dawa kwa ajili ya kuzuia maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

Wakizungumza na mwandishi wa habari hizi jana, baadhi ya watu wanaotumia dawa hizo, walidai tayari wameshatangaziwa mabadiliko hayo, kutoka kupewa bure (kufadhiliwa) na sasa wataanza kuzinunua.

Mmoja wa waathirika ambaye hakutaka jina lake liandikwe gazetini, alisema juzi kuwa alikwenda kuchukua ARV katika hospitali moja ya kanda nchini na kuarifiwa kwamba hivi karibuni wataanza kulipia huduma hiyo.

"Nimeanza kuogopa maana hali itakuwa mbaya sana. Hapa hospitalini walitupa semina juzi (Alhamisi), kwamba, tutakuwa tunanunua ARV dozi ya mwezi mmoja, kwangu hii fedha nyingi sijui itakuwaje," alisema.

**NACOPHA YAFUNGUKA**

Baraza la Taifa la Watu Wanaoishi na VVU (NACOPHA), liliambia Nipashe kuwa tayari wametaarifiwa kuhusu ununuzi wa ARV kwa dozi ya mwezi mmoja, japokuwa hawajaelezwa ni lini utekelezaji wake utaanza.

Akizungumza na mwandishi wa habari hii, Eva Philipo kutoka NACOPHA, alisema baraza hilo lilikuwa kwenye hatua za mwisho za kuanza mradi mpya wa Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Marekani (USAID), ambao umesitishwa.

"Kwa sasa wametupa miezi mitatu ya kupitia misaada yao na baada ya muda huo, tutajua kama wataendelea kutufadhili au la," alisema.

Kuhusu ARV, alisema: "Zinapatikana. Tumeambiwa dawa ni chache kwa hiyo zitaanza kuuzwa kwa Sh. 70,000 kwa dozi ya mwezi mmoja."

Mratibu wa Asasi ya COMPASS, Francis Luwole, na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la DARE, Dk. Lilian Mwakyosi, wanaohusika na afua za kupunguza VVU, walisema wanandoa waliooana mmoja akiwa na VVU na mwingine hana, wataathirika kwa kuwa walikuwa wanatumia dawa kinga za kuzuia maambukizi.

Wengine waliwataja ni wajawazito na wanawake wanaonyonyesha kwa ajili ya kuzuia maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

Luwole alisema dawa hizo zilikuwa zinatolewa kwa ufadhili wa serikali ya Marekani kupitia Mfuko wa PEPFAR.

"Walikuwa wanafadhili ununuzi wa dawa na usambazaji kwa makundi tofauti ambayo yapo kwenye hatari ya kupata maambukizi, wakiwamo wanandoa ambao mmoja ana maambukizi kwa hiyo mmoja alikuwa anatumia hizo dawa ili asiambukizwe," alisema.

Alisema dawa hizo pia, wanapewa watu wanaojichoma dawa za kulevya pamoja na waliobakwa, ili kuzuia maambukizi ya VVU.

"Huduma hii pia, ilikuwa inapatika kwa umma kwa mtu yeyote ambaye anajiona yuko kwenye hatari ya kupata maambukizi alikuwa anaweza kupata hizi dawa. Hili zuio limesimamisha mchakato wote wa hizi huduma," alifafanua.

Alisema mbali ya kusimamisha dawa hizo, kampeni mbalimbali nazo zimesimama ikiwamo uelimishaji rika, ili jamii ione umuhimu wa kupima, kutumia ARV pamoja na kujikinga.

Kutokana na athari hizo, alisema Marekani imetoa mpango maalumu unaojulikana kama WAVER, kurejesha baadhi ya dawa kwa wanawake wanaonyonyesha na wajawazito pekee, ili kuzuia maambukizi kwa mtoto.

"WAVER inaruhusu tu dawa hizo zitolewe kwa wajawazito na wanaonyonyesha, wanufaika wengine wote wamezuiwa. Kwa hiyo ndani ya siku hizi 90 za tangazo la kusimamishwa, hao ndio wanaweza kupata hizi dawa," alisema.

Naye Dk. Mwakyosi alisema, kusitishwa kwa dawa hizo kutazorotesha huduma za afya, kutokana na kuzia watu wengi kupata huduma.

"Athari zipo katika ngazi tofauti tofauti kwa sababu tangazo lilipotoka, lilizuia huduma zote zinazotolewa na Marekani zisimame kwa siku 90 hadi watakapotoa mwongozo. Kwa upande wa VVU, walisimamisha ARV na dawa kinga," alisema.

Hata hivyo, alisema WAVER imeleta unafuu kwa wajawazito na wanaonyonyesha, pamoja na wanaotumia ARV.

"Hii inaweza kuchangia kasi ya kuongezeka kwa maambukizi mapya kwa sababu watu wengi wako kwenye hali ya sintofahamu, lakini pia kuna wimbi kubwa la watu ambao ajira zao zimesitishwa.

"Kwenye huduma za dawa kinga kulikuwa kuna sintofahamu, lakini WAVER jana (juzi), imekuja na taarifa mpya kuruhusu kuwapa wanawake wanaonyonyesha na wajawazito ili kuzuia maambukizi kwa watoto.

"Kwa Tanzania kwenye kununua sina uhakika kama dawa hizi zinaruhusiwa kuuzwa katika maduka ya dawa. Ingeweza kuruhusiwa kuuzwa kwa uangalifu ili wawe wenye uwezo wa kununua wafanye hivyo," alisema Dk. Mwakyosi.

**WAPENDEKEZA SINDANO**

Alipendekeza kuwa serikali inaweza kuruhusu matumizi ya sindano aina ya Lenacapavir inayozuia maambukizi kwa miezi sita mwilini.

Dk. Mwakyosi na Luwole, walitaja dawa kinga zilizozuiliwa kwa makundi mengine ya watu ni vidonge na sindano za PreP pamoja na pete kinga inayowekwa ukeni.

Sindano hiyo inamchanganyiko wa dawa mbili (cabotegravir na rilpivirine), zinazodhibiti kuzaliana kwa VVU pale vinapoingia kwenye mwili ambao umetumia dawa hiyo.

Nyingine ni pete kinga inayojulikana kitaalamu (Dapivirine Vaginal Ring-DVR), inayowekwa ukeni, kwa ajili ya kuzuia maambukizi ya VVU wanawake.

Pete hiyo ya silikoni inavaliwa ukeni na kudumu kwa siku 28, hutoa dawa kinga ya dapivirine ambayo ni aina ya ARV inayozuia VVU kuingia mwilini pale mwanamke anapokutana na mwathirika.

HABARI KITAIFA

# Wakuu SADC, EAC kujifungia Dar kuhusu DRC

**Na Jenifer Gilla**

MARAIS na wakuu wa nchi kutoka Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), leo wanatarajia kukutana jijini Dar es Salaam kuzungumzia mgogoro unaoendelea Mashariki wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Kikao hicho kimetanguliwa na kile kilichoketi jana cha Mawaziri wa Mambo ya Nje ya Nchi wa jumuiya hizo, lengo kuu likiwa kutafuta suluhu ya mapigano kati ya DRC na kundi la M23.

Mkutano huo unatarajiwa kuwakutanisha ana kwa ana kwa mara ya kwanza Rais wa Rwanda, Paul Kagame na Felix Tshisedeki wa DRC tangu kundi la M23 lichukue mji wa Goma. Jumamosi iliyopita, Rais wa Kenya na Mwenyekiti wa sasa wa EAC, William Ruto, alitangaza ushiriki wa viongozi hao katika mkutano huo.

Katika mkutano wa dharura uliofanyika Zimbabwe, Januari 30, mwaka huu, wakuu wa nchi hao walitoa wito wa kufanyika kwa mkutano wa haraka wa pamoja wa wakuu wa nchi za SADC na EAC ili kujadiliana kuhusu hali ya usalama nchini DRC.

Pia walisisitiza kuunga mkono juhudi za kidiplomasia za kupata suluhu la amani kwa mgogoro huo kupitia mchakato wa Luanda, unaoongozwa na João Lourenço, Rais wa Angola na mtetezi mkubwa wa Umoja wa Afrika wa amani na maridhiano barani Afrika na mchakato wa Nairobi, ukiongozwa na Rais wa zamani wa Kenya, Uhuru Kenyatta.

Mkutano huo pia uliazimia mawaziri wa ulinzi na wakuu wa ulinzi kwa nchi zinazochangia wanajeshi nchini DRC kwenda nchini humo kuhakikisha wanajeshi wa ujumbe wa SADC waliopo DRC (SAMIDRC) wako salama na kuwarejesha nyumbani wanajeshi waliofariki dunia na wale waliojeruhiwa.

Zikiwa zimepita siku tatu tangu kundi la M23 kutangaza kusitisha mapigano, juzi limeuteka Mji wa Nyabibwe ulioko kwenye ukingo wa Ziwa Kivu, Jimbo la Kivu Kusini nchini DRC likidai kujihami na mashambulizi ya Jeshi la Serikali ya DRC.

Kwa mujibu wa Umoja wa Mataifa, mapigano kati ya waasi FARDC, yameleta madhara kwa binadamu katika Mji wa Goma sambamba na kuleta uharibifu wa miundombinu ikiwamo makazi na nishati.

Ofisi ya Umoja wa Mataifa inayoshughulikia masuala ya kibinadamu inakadiria kuwa hadi kufikia, Februari 5, mwaka jana, mapigano hayo yalisababisha vifo zaidi ya 2,800 katika Mji wa Goma nchini humo.

Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC) ilitoa taarifa kuwa inafuatilia kwa ukaribu yanayoendelea nchini DRC na uwezekano wa kuwapo uhalifu wa kivita eneo hilo.

Akizungumza na vyombo vya habari juzi, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), António Guterres, alitoa rai kuwa mkutano huo uje na suluhu kuhusu hali ya mashaka inayoendelea DRC.



Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Jaji wa Rufani, Jacobs Mwambegele (kulia), akikagua mafunzo ya vitendo ya Waandishi Wasaidizi ngazi ya Jimbo kutoka Halmashauri ya Jiji la Tanga, katika siku ya pili ya mafunzo jana, kwa ajili ya maandalizi ya zoezi la Uboreshaji Daftari la Kudumu la Wapigakura linalotarajiwa kufanyika katika mikoa ya Tanga na Pwani kuanzia Februari 13 hadi 19, mwaka huu. **PICHA: INEC**

# Bunge laazimia ukusanyaji kodi pango ardhi ufanywe na wizara

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeazimia serikali irudishe ukusanyaji wa kodi ya pango la ardhi ili kufanywa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kutokana na halmashauri kutotekeleza jukumu hilo kwa ufanisi.

Limeazimia wizara hiyo kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) isimamie halmashauri kurejesha Sh. bilioni 22.5 zilizokopeshwa kwenye mradi wa kupanga, kupima na kumilikisha ardhi baada ya kubainika asilimia 70 ya halmashauri na taasisi zimeshindwa kurejesha tangu mwaka 2018.

Pamoja na hayo, limelitaja Jiji la Dodoma kuwa moja ya sehemu zenye migogoro mingi ya ardhi nchini na inachangiwa na uwapo wa watumishi wasio waaminifu na wasiozingatia sheria katika sekta ya ardhi.

Akiwasilisha bungeni jana taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati ya Bunge, Ardhi, Maliasili na Utalii, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Timotheo Mnzava, alisema serikali iliamua ukusanyaji wa kodi ya pango la ardhi ufanywe na Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini.

Mnzava alisema lengo ni kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato yatokanayo na pango la ardhi na uamuzi huo umetoa matokeo hasi katika ufuatiliaji wa makusanyo hayo.

Alisema wizara haina fedha za kutosha kwa ajili ya shughuli hiyo na halmashauri ambazo zimepewa jukumu hilo hazilitekelezi.

"Bunge linaazimia serikali irudishe jukumu la ukusanyaji wa kodi ya pango la ardhi katika wizara hii ambayo ndio ina nyezo za kisheria na kimfumo katika kutekeleza jukumu hilo," alisema.

Pia alisema Wizara ya Ardhi iwezeshwe fedha katika kutimiza jukumu hilo kwa kuruhusu ibaki na asilimia 20 ya makusanyo ya kodi ya kwa ajili ya kuongeza ufanisi.

Kuhusu Mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi nchini, Mwenyekiti huyo, alisema kutokana na halmashauri na taasisi zilizokopeshwa fedha kushindwa kurejesha hali hiyo inakwamisha azma ya serikali ya kupanga na kupima ardhi yote nchini.

"Bunge linaazimia serikali kupitia Wizara ya Ardhi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-TAMISEMI ihakikishe inazisimamia halmashauri zote kurudisha kiasi cha Sh. bilioni 22.5 walizokopeshwa kwenye mradi huu, ili ziweze kutumiwa na wizara ya sekta katika kuendelea kupanga, kupima na kumilikisha ardhi kwenye halmashauri zote nchini," alisema.

Aidha, limeazimia kwamba wizara hiyo ihakikishe inafanya uchambuzi wa maandiko ya halmashauri zinazoomba mikopo kupitia programu hiyo ili kujiridhisha kama zinauwezo wa kurejesha fedha hizo. Pia Bunge limeazimia kupitia Wizara ya Ardhi ihakikishe inalinda uhai wa Mfuko wa Mzunguko wa Maendeleo ya Ardhi (Plot Development Revolving Fund) ili uendelee kuwa chanzo cha uhakika cha fedha kwa ajili ya programu hiyo.

Kuhusu ardhi ya wawekezaji ambayo haijaendelezwa, alisema kamati imebaini uwapo wa uhaba wa ardhi kwa wananchi wanaoishi kuzunguka baadhi ya maeneo ambayo yako chini ya wawekezaji wenye mashamba makubwa, huku yakiwa haijaendelezwa kwa mujibu wa sheria.

Alisema hali hiyo inayochangia migogoro inayosababisha maafa, majeruhi na uharibifu wa miundombinu kati ya wawekezaji na wananchi katika maeneo husika.

"Bunge linaazimia kwamba, serikali ifanyetathmini ya wamiliki wa mashamba makubwa yote nchini ili kutambua ambayo hajaendelezwa na kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa sheria," alisema.

# Vigogo matatani uchepushaji maji

**Na Daniel Limbe,** CHATO

BAADHI ya viongozi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Chato (CHAWASA) wameingia matatani kwa tuhuma za kuchepusha mifumo ya maji na kuyaingiza kwenye mashamba yao ya mpunga kinyume cha sheria.

Licha ya kuwapo kwa malalamiko ya mara kwa mara kuhusu wananchi kukosa huduma hiyo kwa takribani miaka miwili na wengine wakipata maji kwa mgawo unaotajwa kutokueleweka ukomo wake, imebainika mengi huelekezwa katika mashamba ya vigogo hao.

Nipashe ilifika katika eneo la tukio ambapo baadhi ya wananchi akiwamo, Leonard Shilengwa, alisema katika Kitongoji cha Mtakuja B, Kata ya Muunganowila, vigogo hao wamekuwa wakitumia maji hayo bila hata mita ya kuhesabu ankala.

Naye John Daud, alidai wamekuwa wakitekeleza hujuma hiyo kwa muda mrefu wa misimu mitatu ya kilimo ukiwahusisha watumishi wa mamlaka hiyo (majina tunayahifadhi) kujinufaisha kwa maslahi binafsi kinyume cha sheria, ambapo kigogo mmoja akimwagilia takribani hekari 10 za shamba la mpunga na mwingine akiwa na hekari tano.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kahumo, Paulo Manyilizu, alisema changamoto kubwa ya uhaba wa maji imekuwa ikiwakumba watumishi wa Zahanati ya Nyabilezi, uwanja wa ndege wa Geita ulioko Chato pamoja na wakazi wa Kijiji cha Buzirayombo, ambao wanahudumiwa kupitia bomba hilo.

"Baada ya kubaini wizi huu wa maji nimewasiliana na watumishi wa Kituo cha Afya Nyabilezi nao wamekiri hakuna maji kituoni hapo, maji yote yameelekezwa kwenye mashamba haya," amesema.

Alisema watumiaji 11 walilipia kila mmoja Sh. 120,000 tangu mwaka 2022 ili waunganishiwe huduma ya maji kwenye kijiji chao na Waziri wa Maji katika ziara yake wilayani humo mwaka jana aliagiza wananchi wapewe huduma ya maji.

Alisema licha ya maagizo hayo mpaka sasa hakuna kilichofanyika zaidi ya kuambiwa jambo hilo linashughulikiwa.

Diwani wa Muungano, Charles Kapembe, alisema mchezo huo wa kuhujumu miundombinu ya maji kwenye kata hiyo huenda ndiyo chanzo cha wananchi wake kukosa huduma ya majisafi na salama. Alisema hali hiyo imesababisha adha kubwa kwa jamii baada ya kutumia gharama kubwa kujitibu magonjwa ya matumbo.

Akijibu tuhuma zilizoelekezwa dhidi ya mamlaka yake, Mkurugenzi Mtendaji wa CHAWASA, Mhandisi Isack Mgeni, alikiri kuwapo kwa wizi wa maji uliofanywa na sehemu ya viongozi wa mamlaka.

Alisema tuhuma hizo zinamhusisha mtumishi mmoja wa mamlaka hiyo pamoja na aliyekuwa Mkurugenzi wake kabla ya uteuzi wake kutenguliwa mwaka jana na kwamba, hatua za awali zimeanza kuchukuliwa kwa watuhumiwa hao.

Alisema mtumishi huyo amekamatwa na Jeshi la Polisi kwa mahojiano zaidi na kwamba mamlaka hiyo inaandaa utaratibu wa kumsimamisha kazi kabla ya uamuzi mwingine kuchukuliwa, huku taratibu nyingine zikiandaliwa kuhusu aliyewahi kuwa mkurugenzi.

RIPOTI MAALUM

# Wazazi wacharuka wanafunzi wa Darasa la IV kusoma hadi usiku

**Na Jenifer Gilla**

BAADHI ya shule binafsi ambazo zinawataka wanafunzi wa darasa la nne kukaa bweni kwa kigezo cha kuwafundisha hadi usiku, kimewaibua wazazi na walezi wakipinga uamuzi huo.

Wazazi wengi wamejenga hoja kwamba umri wa watoto wa darasa la nne ni mdogo kukaa bweni na hata suala la kuamka na kujisimamia bado ni mtihani kwao.

Wengine wanasema pia katika baadhi ya shule hizo binafsi kuna utaratibu mwingine ulioanzishwa wa kufundisha watoto wa darasa la saba hadi siku ya Jumapili, wanaouna kuwa si sahihi kwa afya za watoto hao, kwani hawapati muda wa kutosha wa kupumzika.

Wakati hayo yanaendelea, Mtaala wa Elimu ya Msingi unaelekeza muda wa masomo kwa siku kwa wanafunzi wa darasa tatu hadi la sita kuwa ni siku sita kwa kipindi kimoja, sawa na saa 40 na idadi ya vipindi kwa siku ni nane na kwa wiki ni 38.

Baadhi ya walimu shule binafsi wamefunguka kuwa hizo ni moja ya mbinu kuhakikisha shule kuwa na matokeo mazuri ambayo ndiyo humfanya mwalimu kuendelea kufanya kazi katika shule husika, kinyume cha hapo kibarua kitakuwa hatarini.

Kutokana na hayo yanayoendelea, serikali imesema kitendo hicho ni kinyume cha sheria na si haki kwa mtoto wa darasa hilo kukaa bweni au kusoma kwa zaidi ya saa za kisheria kwa sababu anapaswa kupumzika na hata kuitumia likizo yake.

Baadhi ya wazazi wameandika katika mtandao wa kijamii wa Instagram akiwamo mzazi mmoja ambaye anaeleza namna walimu wa shule anayosoma mtoto wake wa darasa la nne wamemwambia amhamishie bweni au awajibike kila siku kumfuata saa 2:00 usiku kwa maana ndio muda ambao masomo yanamalizika.

Anasema hakubaliani na hilo kwa sababu anaamini kwa umri wa mtoto wake (bila kuutaja) bado anastahili kukaa chini ya uangalizi wake lakini pia haoni haja ya watoto kusoma mpaka saa mbili usiku.

Kutokana na sintofahamu hiyo, mwandishi wa habari hii amezungumza na wazazi wengine wa watoto walio darasa la nne katika shule mbalimbali akiwamo mzazi (jina linahifadhiwa) mwenye mtoto wa miaka 10 anayesoma moja ya shule binafsi zilizoko Tabata, Dar es Salaam, ambaye anaungana na wenzake kupinga hilo.

Mzazi huyo anakiri mwishoni mwa mwaka jana alipokea barua kutoka katika uongozi wa shule ikimtaarifu kusudio la kumwamishia mtoto wake bweni kuanzia mwezi Januari, mwaka huu.

Hata hivyo, anasema hakukubaliana na uamuzi huo, hivyo shule zilipofunguliwa alikwenda kuzungumza na mkuu wa shule akamkubalia ombi lake la kutokaa bweni, ingawa ametakiwa kuhakikisha kila siku mtoto anafika shuleni saa 12:00 asubuhi na muda wa kumchukua ni saa mbili usiku.

"Ratiba hii inaniumiza kama mzazi kwa sababu ninaona mtoto bado ni mdogo, hivyo kuingizwa katika ratiba kama hii anakosa haki nyingine za msingi kama vile kucheza.



Kanishna wa Elimu, Dk. Lyabwene Mtahabwa



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda

Dickson Mmasy, anasema alilazimika kumhamishia mtoto wake bweni ili kufuata matakwa ya shule, lakini hakubaliani na uamuzi huo kwa kuwa watoto ni wadogo na hawawezi kujisimamia.

"Wiki mbili zilizopita nilikwenda kumtembelea mtoto shuleni na kumkuta na mapunye, hali inayoonesha kuwa hata wasimamizi wa watoto hao hawafanyi kazi yao vizuri.

"Ni vile tu ni vigumu kuhamisha mtoto wa darasa la nne kwa kuwa ana mtihani wa taifa, ila ningeshamhamisha mapema kwa sababu hata mimi mzazi silali kwa amani nyumbani. Mawazo yote yako kwa mtoto," anasema.

Mzazi wa mtoto anayesoma darasa la saba, Agnes Mnyika, amelalamikia shule anayosoma kijana wake kufundisha hadi siku ya Jumapili.

"Elimu siku hizi imezidi, ni mwezi mmoja tu, lakini tayari mtoto amekonda, masomo gani hayo ya siku saba kwa wiki. Ina maana mtoto wa darasa la saba hatakiwi kupumzika. Tunafanya watoto wachukie shule mapema," anasema.

**WATAFUTA UFAULU**

Mwalimu wa Shule ya Msingi Range iliyoko Iringa, Melina Mgata, anasema lengo la kuwaweka bweni wanafunzi wa darasa la nne ni kutafuta ufaulu mzuri.

Anasema mtoto wa darasa la nne asipokuwa katika mazingira hayo, anaweza asipate muda wa kusoma, akaendekeza michezo nyumbani, hivyo kuchangia kutofanya vizuri katika mtihani wa taifa.

"Wanaokaa bwenini wanafaulu vizuri kwa sababu wanapata muda mwingi wa kujisomea tofauti na yule anayekaa nyumbani," anadai.

Kuhusu umri unaolalamikiwa kuwa mdogo kukaa bweni, mwalimu huyo anasema inategemeana na imani ya mzazi, lakini zipo baadhi ya shule kuna watoto wadogo zaidi wanakaa bweni na wanasoma vizuri.

Anasema ziko baadhi ya shule ni lazima mtoto akae bweni na nyingine wanasheria zao kama mzazi hawezi kukubali mtoto akakaa huko hawampokei. Hata hivyo, mwalimu huyo anapinga sio kweli kwamba kila shule inalazimisha mwanafunzi akae bweni, ziko ambazo hazifanyi hivyo na wazazi wanaweza kufanya chaguo.

Mwalimu wa Shule ya Msingi Group Side Academy, Kimara Suka, Dar es Salaam, Fortinatus Lufyagila, anasisitiza kuwa lengo la kufanya hivyo ni kuwa na mgawanyo wa muda na kuwabana wanafunzi kusoma kwa kuwa darasa hilo ni la mtihani wa taifa.

Anafafanua kuwa kwa upande wa shule za binafsi matokeo ndio yanamfanya mwalimu aendelee kufanya kazi katika shule husika, kinyume na hapo kibarua kitakuwa hatarini, ndio maana wanalazimika kubuni mbinu za kuwawezesha wanafunzi kufaulu.

"Wazazi wanaolaumu wanahaki kulingana na umri wa watoto wanapaswa kukaa nyumbani, lakini pia akumbuke kuna masuala ya matokeo mtoto wake akifeli asitafute mtu wa kumlaumu.

"Kwa sababu kumekuwa na kasumba mtoto akifeli mzazi anaanza kulalamika, 'mimi ninatoa ada kubwa halafu mtoto anafeli," anasema Lufyagila.

**MWENYEKITI SHULE BINAFSI**

Mwenyekiti wa Shule Binafsi Kanda ya Kaskazini, Reonald Mau, anasema si kweli shule binafsi zinalazimisha wanafunzi wa darasa la nne kukaa bweni bali kinachofanyika ni makubaliano kati ya shule husika na kamati ya shule na wazazi.

Anasema kamati za shule huwa zinakaa kupanga na kuitisha mkutano wa wazazi kisha wanakubaliana wazazi, walimu na mamlaka za shule.

"Shule nyingi za binafsi na hizo zinazofundisha mchepuo wa Kingereza zinasomesha watoto kutoka maeneo mbalimbali. Maana yake kuna wazazi wengine wanahitaji watoto wakae bweni kuanzia darasa la kwanza na wanaamini kwamba, huko ndiko wanapatiwa huduma vizuri.

"Hayo malalamiko hakuna nguvu inayotumika, kama inatokea mzazi analalamika labda atakuwa na shida zake mwenyewe. "Lakini pia, kwa mzazi asiyetaka mtoto akae bweni (tukumbuke) karibu shule zote binafsi zina magari ya shule, kwa mzazi asiyetaka mtoto wake akae bweni, anaweza kulipia usafiri huo mtoto akawa anachukuliwa asubuhi na kurudishwa jioni kila siku," anafafanua.

Anasisitiza kuwa wako wanafunzi wanaokaa bweni kuanzia darasa la kwanza, kikubwa mzazi anachotakiwa kuhakikisha ni usalama wa mtoto katika mazingira anayosoma.

"Huwa hatulazimishi, kunakuwa na makubaliano na palipo na makubaliano huwa hakuna shida na mzazi anayekuwa haridhiki huwa tunamshauri atafute shule nyingine," anasema Mau.

**WADAU WANG'AKA**

Kupitia mtandao wa kijamii wa Instagram, Bakari Mazengo, aliandika kuwa shule ya binafsi inayojitengenezea mazingira mazuri ili iwe na matokeo mazuri kwenye mtihani wa taifa.

Anasema kwamba kama mzazi anaona mazingira ya shule hiyo sio rafiki kwake na kwa mtoto, njia rahisi ni kutafuta shule itakayomfaa kwa mazingira yake.

"Kuwalalamikia na kuwatuhumu ni kufifisha jitihada zao kutengeneza matokeo mazuri ambayo ndio kivutio chetu kwenye shule zao," anasema Mazengo.

Juma Mubaraka, anasema si shule zote zinalazimisha watoto wa darasa la nne kukaa shule za bweni.

"Kama unaona huwezi waambie, ataingia na kutoka muda wa kawaida na akiwa nyumbani utamsimamia mwenyewe kujisomea maana wengine shuleni wataendelea kujisomea.

Dimoso Robert, anasema watoto wake hawatokaa bweni labda mpaka watakapofika kidato cha tano na kuendelea, akisisitiza ataangalia.

Isha Mahanga, kwa upande wake, anaona mpango huo una lengo la kuharibu watoto na kusisitiza mtoto wa darasa la nne hawezi hata kuamka peke yake.

**HATUA ZA SERIKALI**

Kamishna wa Elimu, Dk. Lyabwene Mtahabwa, alisema kitendo hicho ni kinyume cha sheria na si haki kwa mtoto wa darasa hilo, kukaa bweni au kusoma kwa zaidi ya saa za kisheria kwa sababu anapaswa kupumzika na hata kuitumia likizo yake.

"Tunahimiza kila shule izingatie kalenda ya mihula na anayeenda kinyume lazima ishughulike naye, maana watoto nao jamani wanahitaji muda wa kupumzika pamoja na familia zao," alisema na kuomba jina la shule inayofanya hivyo ili kufuatilia na kuuchukulia hatua za kisheria uongozi wake.

"Si sawa hata kidogo na tulishapiga marufuku, haikubaliki kabisa na tutafanya ufuatiliaji," alisisitiza.

Pia alisema kitendo cha shule kumtaka mzazi asiyetaka mtoto wake kukaa bweni na kumpa sharti la kumpeleka asubuhi na kumfuata usiku, si sawa na haitakiwi kuwa hivyo kwa kujibu wa sheria.

## Matatani madai kula fedha soko la mazao

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

KAMANDA wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Marko Chilya, amemwagiza Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Songea (OCD) kuwakamata viongozi wa Chama cha Wafanyabiashara wa Soko la Mazao (UWAMASA) ambao wanadaiwa kula fedha zaidi ya Sh. milioni 90 ambazo baadhi walikopesha viongozi wa chama hicho.

Alitoa maagizo hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari, ambapo alisema taarifa hiyo ilikuwa haijafika ofisini kwake na kulazimika kumtafuta Mkuu wa Polisi wa Wilaya hiyo.

Alisema alipata taarifa kuwa umoja wa wafanyabiashara wa soko la mazao lililoko Msamala Manispaa ya Songea, ulileta taharuki kubwa wakati wanachama wakiudai uongozi wao.

Alisema wafanyabiashara hao walikuwa wakidai uongozi wao uwapatiwe gawio la Sh. 300,000 kwa kila mwanachama, fedha ambazo zingewasaidia kununulia pembejeo na ada za shule za watoto wao.

Alisema baada ya kupata taarifa kuwa kuna watu wamejaa kituo cha polisi ambao ni wafanyabiashara wakidai uongozi wao umewaibia fedha, ndipo alipoanza ufuatiliaji.

Alisema baada ya ufuatiliaji alibaini uongozi wa umoja huo, walikwenda kwa Mkuu wa Polisi Wilaya ambaye aliwaachia kwa dhamana na kuwataka warudishe fedha, jambo ambalo lilizua taharuki kwa wafanyabiashara.

Kutokana na hilo, Kamanda huyo alisema alimwagiza Mkuu wa Polisi Wilaya kuwakamata, kuwahoji na kuona namna ya kuwachukulia hatua.

Baadhi ya wafanyabiashara wakizungumza na Nipashe katika soko la mazao lililoko Msamala Manispaa ya Songea, walisema kwa muda mrefu wamekuwa wakiomba kuitishwa mkutano mkuu wa umoja huo ambao uliitishwa Januari 30, mwaka huu. Joseph Komba alisema uongozi wa umoja huo unadaiwa kuwaibia fedha zaidi ya Sh. milioni 90 ambazo walichangishana ili ziweze kuwasaidia kununua pembejeo pamoja na kulipa ada kwa watoto wao, jambo ambalo limeonekana kuwa ni tatizo kubwa. Komba alisema wanachama walikuwa wakidai kwa muda mrefu kuitisha mkutano mkuu ili wasomewe mapato na matumizi lakini walikuwa wakipigwa chenga.

Athuman Msalipanda alisema pamoja na kuwapo kwa malalamiko hayo bado kuna tatizo kubwa la wanachama kutowekwa wazi kuhusu fedha hizo.

Msalipanda aliomba vyombo vya dola ikiwamo TAKUKURU kuingilia kati kwa lengo la kuubaini ubadhirifu wa fedha hizo za wanachama.

Mwenyekiti wa umoja huo, Bakari Naheka, alipotafutwa na mwandishi wa habari hii kuhusiana na malalamiko hayo alikiri kuwa kwenye akaunti yao ya benki kulikuwa na zaidi ya Sh. milioni 79.

Alisema wamelipa Sh. milioni 20 na wanadaiwa Sh. milioni 59, fedha ambazo zinatarajiwa kulipwa Februari 22, mwaka huu.

Katibu Mkuu wa Umoja huo, Charles Swila, aliwaomba wafanyabiashara wenzake ambao ni wanachama zaidi ya 250 wawe na subira wakati wanafanya jitihada za kuzirejesha fedha wanazodai.

# DAWASA yaandika historia mpya bwawa la Kidunda

**Na Frank Monyo,** MOROGORO

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) imeweka historia kwa kuanza utekelezaji wa Mradi wa Bwawa la Kidunda, lililoko Wilaya ya Morogoro, ambalo linatarajiwa kuhifadhi lita bilioni 190.

Mradi huo ambao umekuwa katika mipango ya maendeleo tangu Tanzania ilipopata Uhuru mwaka 1961, hatimaye unatekelezwa kwa vitendo chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kutumia fedha za ndani.

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Mhandisi Mkama Bwire, alisema hayo jana wakati wa ziara ya watendaji wa DAWASA, wahariri wa vyombo vya habari na waandishi wa habari waliotembelea mradi huo ili kujionea maendeleo yake.

"Bwawa hili limekuwa katika mipango kwa zaidi ya miongo sita, lakini sasa DAWASA kupitia serikali ya awamu ya sita imelifanikisha. Tayari mradi huu umekwishafikia zaidi ya asilimia 27 ya utekelezaji," alisema Bwire. Aliongeza kuwa mradi huo unaogharimu zaidi ya Shilingi bilioni 336, unalenga kuhakikisha upatikanaji wa maji wa uhakika kwa wakazi wa mikoa ya Morogoro, Dar es Salaam, na Pwani kupitia chanzo cha Mto Ruvu. Utekelezaji wake unatarajiwa kukamilika ifikapo Desemba 2026.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri, Deodatus Balile, alipongeza DAWASA kwa hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi huo muhimu.

"Mradi huu ni wa kihistoria na unakwenda kutatua changamoto ya upatikanaji wa maji katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani. Faida zake ni kubwa, na ifikapo Juni 2026, inatarajiwa tatizo la mgawo wa maji litakuwa historia, hasa kutokana na kuongezeka kwa upatikanaji wa maji kutoka Mto Ruvu," alisema Balile.

Meneja wa Mradi wa Bwawa la Kidunda, Christian Christopher, alisema bwawa hilo litasaidia kupunguza uhaba wa maji kama ule ulioshuhudiwa wakati wa ukame wa miaka 1997, 2021, na 2022. Katika vipindi hivyo, viwango vya maji katika vyanzo vya Ruvu Juu na Chini vilishuka sana na kusababisha mashine kuzimwa.

"Kwa bwawa hili, tutaweza kudhibiti mtiririko wa maji hasa wakati wa mvua na vipindi vya ukame," alisema Christopher.

Mradi huo unajumuisha ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa megawati 20 na laini ya kusambaza umeme ya kilovolti 132. Pia utahusisha ujenzi wa barabara ya changarawe yenye urefu wa kilomita 75.

Christopher alisema mradi huo umezalisha zaidi ya ajira 2,200 na unatarajiwa kukamilika ifikapo Juni 2026.

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Maji ya Bonde la Wami/Ruvu, Janeth Kisoma, alisema bodi hiyo iko katika hatua za mwisho za kutangaza eneo la Bwawa la Kidunda kuwa chanzo cha maji na eneo la ardhi oevu. Uteuzi huo utaiwezesha mamlaka kutekeleza sheria za kulinda na kuhifadhi eneo hilo.

Mradi wa Bwawa la Kidunda unatarajiwa kuwa suluhisho la muda mrefu kwa changamoto ya maji, huku ukichangia pia katika uhifadhi wa mazingira na maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika mikoa inayonufaika.



Mkurugenzi wa Shirika la Akili Platform Tanzania (APT), Roghat Robert (kushoto), akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Msingi Isike mjini Tabora mapema wiki hii, alipokuwa akitoa elimu kuhusu athari za ukatili wa kijinsia na afya ya akili. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wataka uchimbaji visima kila jimbo ukamilishwe

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeazimia mambo 11 yanayohusu maji na mazingira ikiwamo Wizara ya Maji kukamilisha mchakato wa uchimbaji wa visima vitano kwa kila jimbo kama ilivyoahidiwa na serikali.

Kadhalika. utiririshaji wa majitaka na taka za viwandani katika Ziwa Victoria umetajwa kusababisha kupungua kwa samaki, kuongezeka kwa viumbe vamizi, kuharibika kwa mifumo ikolojia muhimu ya viumbe hai vya majini na kupungua kwa ubora wa maji.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Jackson Kiswaga, aliyasema hayo jana bungeni wakati akiwasilisha taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati ya Bunge ya Maji na Mazingira.

Alisema baadhi ya visima vinavyoendelea kuchimbwa vimekuwa vikikosa maji licha ya kutumia rasilimali nyingi katika uchimbaji huo.

Kiswaga alisema hali hiyo inasababisha hasara na kurudisha nyuma juhudi za kusaidia upatikanaji wa maji kwa maeneo yote nchini na Bunge linaazimia kwa kushirikiana na wadau wa utafiti (vyuo vikuu, TPDC) serikali iboreshe utafiti kwenye utafutaji wa maji chini ya ardhi kwa kuwaongezea uwezo wataalamu wake pamoja na kutumia teknolojia za kisasa katika uchimbaji wa visima.

Alisisitiza Wizara ya Maji ichukue hatua madhubuti zitakazowezesha kukamilika kwa uchimbaji wa visima vitano kwa kila jimbo.

Alisema pia, Bunge linaazimia kuanzishwa kwa kamati ya kitaifa itakayoratibu shughuli za uchimbaji wa mabwawa ya maji kwa kuzingatia uhitaji wa maji kwa shughuli mbalimbali za kijamii na kiuchumi.

Alisema licha ya hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kuhusu utiririshaji wa majitaka na taka za viwandani katika ziwa hilo, bado unaendelea kwa baadhi ya maeneo ikiwamo mto Milongo.

Alisema ziwa hilo limeendelea kuathiriwa na shughuli zisizo endelevu za kibinadamu zikiwamo; uvuvi haramu, uharibifu wa maeneo oevu, kilimo kisichozingatia uhifadhi, uchimbaji madini usiokuwa endelevu.

Alitaka halmashauri zote zinazozunguka Ziwa Victoria kutekeleza mikakati iliyoko ya udhibiti wa taka katika ziwa hilo kwa kuzingatia ipasavyo Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.

"Ofisi ya Makamu wa Rais ichukue hatua za haraka zitakazowezesha udhibiti endelevu wa utiririshaji wa majitaka katika Mto Milongo ulioko jijini Mwanza," alisema.

Kiswaga alisema kutokana na majanga yaliyoyakumba maeneo ya Hanang, Kibiti na Rufiji, Bunge linaazimia itungwe sheria, kanuni na miongozo ya uanzishaji wa mfuko wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi.

Alisema mfuko huo utagharamia utekelezaji wa mipango na mikakati ya usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi nchini.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uteuzi wachezaji Stars CHAN usiwe ni Simba, Yanga pekee

**TIMU** ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), ni moja ya timu zilizofuvu kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN 2025).

Fainali za michuano hiyo inayoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), itafanyika kuanzia Agosti 2 hadi 30, mwaka huu kwa ushirikiano wa pamoja wa Tanzania, Kenya na Uganda.

Katika kuhakikisha Taifa Stars inafanya vyema katika fainali hizo ambazo zitakuwa ni mwendelezo wa timu itakayopeperusha bendera ya Tanzania katika fainali za AFCON zitakazochezwa baadaye Desemba, mwaka huu, ni lazima benchi la ufundi liongeze umakini wa uteuzi wa wachezaji.

Uteuzi wa wachezaji ndio hutoa picha ya mapema ya wapi timu itakwenda, tunahitaji kuona sasa Taifa Stars inapata matokeo chanya katika michuano huyo na kuacha tabia ya kuwa wasindikizaji.

Tofauti na fainali nyingine zinazofanyika, mwaka huu michuano hiyo inachezwa kwenye ardhi ya nyumbani, hii inamaanisha kufanya vyema kwa timu yetu kutawapa furaha zaidi mashabiki na kuacha unyonge wa kushangilia mataifa mengine yaliyotuzidi.

Kama wenzetu wanafanikiwa kwa kubeba mataji au angalau kucheza hatua ya nusu fainali mara kwa mara, si dhambi na sisi makocha wetu wakaiba au wakageuza kile ambacho wanakifanya ili kuvuna matokeo mazuri.

Wakati Ligi Kuu Tanzania Bara imeingia mzunguko wa lala salama na ndio inayotoa idadi kubwa ya nyota watakaoshiriki michuano hiyo, huu ni wakati kwa makocha kuhakikisha wanaangalia wachezaji ambao watakuwa na uwezo wa juu wa kubeba jukumu la kuipeperusha vyema bendera ya nchi yetu kwenye fainali hizo.

Mbali na ligi hiyo, pia Ligi ya Championship isisahaulike, benchi la ufundi la Taifa Stars linatakiwa kutupia macho kwa kusaka wachezaji ambao wana uwezo wa kujiunga na kikosi hicho, huu tena si wakati wa kuita wachezaji kwa kuangalia ukubwa wa timu au majina yao.

Benchi la ufundi linatakiwa kuangalia uwezo husika wa mchezaji ili kupata timu imara itakayotupeleka katika kufikia malengo na si kuita wachezaji kwa mazoea au kwa kuangalia kutoka kwa vigogo, Simba na Yanga.

Kama mshambuliaji, Selemani Mwalimu, wa Fountain Gate FC ya Manyara, ameonekana na Wydad AC ya Morocco, basi Kocha Mkuu wa Stars, Hemed Suleiman na wasaidizi wako, mnajukumu la kuzunguka Tanzania nzima ili kutafuta wachezaji watakaoibeba nchi na kuacha kukariri nyota wale wale tuliowazoea.

Wachezaji wanaotakiwa kuitwa katika kikosi hicho ni wale wanaopata namba kila siku kwenye vikosi vyao na si vinginevyo, mchezaji ambaye hachezi kila siku hawezi kuwa msaada sahihi kwa nchi, fainali za CHAN ni michuano yenye ushindani zaidi kwa sababu nyota wanaokutana wanajiweka sokoni kwa ajili ya kusaka timu za Ulaya.

Kama ambavyo timu kutoka Afrika Magharibi, Afrika ya Kaskazini na Kusini zimekuwa zikiogopewa, umefika wakati kwa wawakilishi wa Afrika Mashariki pia kuogopewa, na ili kufikia hatua hii, makocha wake wanatakiwa kuongeza umakini kwenye kuteua wachezaji.

Tunawakumbusha pia wachezaji watakaopata nafasi hiyo kutambua wanakwenda kuwakilisha Watanzania zaidi ya milioni 60, hivyo wakajitume na kucheza kwa nidhamu wakati wote.

Tunaamini maandalizi mazuri ambayo Taifa Stars itayapata kuelekea CHAN, itakuwa ni mwendelezo wa kuwa na kikosi imara kitakachoshiriki Fainali za AFCON hapo Desemba, ingawa hapo watajumuishwa na nyota wanaocheza nje ya Tanzania.

Wachezaji ambao wamepita katika misingi sahihi, wanapewa nafasi ya kuipa timu matokeo chanya, tunaamini hili litafanyika kwa sababu kwa sasa Tanzania imekuwa ni timu inayoingia kama mshindani na si wasindikizaji kama ilivyokuwa ikijulikana miaka ya nyuma.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Simba imsamehe Chasambi, atambue yuko timu kubwa

**KWA** sasa mjadala mkubwa katika habari za michezo ni jinsi mchezaji chipukizi wa Simba, Ladack Chasambi, alivyojifunga kwenye mchezo wa Ligi Kuu kati ya timu yake dhidi ya Fountain Gate.

Kila mmoja anaongea lake, wapo wanaomtetea na wengine waliomlaumu na kumshutumu. Hiyo ni baada ya mchezo uliopigwa kwenye Uwanja wa Tanzanite Kwaraa ulioko Babati, mkoani Manyara. Alifunga bao ambalo lilikuwa la kusawazisha kwa wapinzani wa Simba, Fountain Gate. Mechi ikaisha kwa sare ya bao 1-1.

Awali Simba ilikuwa ina bao moja lililofungwa na Leonel Ateba. Nadhani kilichowauma zaidi wanachama na mashabiki wa Simba si matokeo ya sare tu, bali kushindwa kupanda tena kileleni na kumwacha Yanga akiongoza kwa pointi 45, dhidi ya 44 walizonazo wao.

Jinsi alivyolifunga bao hilo pia kumezidisha gumzo na mjadala. Alipewa mpira wakiwa mbali, karibu na katikati ya uwanja. Hakuwa amekabwa wala kubanwa na mtu yoyote.

Angeweza kugeuka na kwenda mbele, au kutafuta mchezaji mwenzake jirani ili ampasie. Alichofanya akapiga shuti kubwa la juu kuelekea langoni mwake. Wakati huo kipa, Moussa Camara, alikuwa ametoka langoni, kwa sababu yeye ndiye aliyeuanzisha mpira huo.

Kwa maana hiyo hata ulipokuwa ukielekea langoni pale alipokuwa hakuwa na uwezo wa kuudaka kwa mikono kwa sababu alikuwa amerudishiwa na mchezaji wake mwenyewe. Kibaya zaidi ulipigwa juu, ukiwa na nguvu kubwa na kasi, hivyo ulimshinda, ukajaa wavuni na kushangaza wengi uwanjani hapo.

Wanaomtetea, wanasema makosa kama yale hufanyika kwenye michezo mingi katika mpira wa miguu duniani. Mpira wa miguu ni mchezo wa makosa, hivyo linapofanyika ndipo goli linapofungwa.

Wengine wakaenda mbali zaidi na kusema kosa alilofanya litamfanya kumjenga na kumkomaza, likimfanya kuwa makini zaidi katika michezo inayofuata.

Wanaomlaumu wanaleta hoja hakuwa na haja yoyote ya kurudisha mpira kwa umbali mrefu ule kurudi kwa kipa wakati ambapo Simba inasaka bao la pili ili kuua mechi.

Wanasema hakuwa kwenye shinikizo lolote na wala hakuwa karibu na lango. Wakakumbushia mabao aliyokuwa akisababisha Fondoh Che Malone afadhali alikuwa karibu na lango na akiwa amezongwa na wachezaji wa timu pinzani, lakini kwa Chasambi, lilikuwa ni kama bao la kujitakia.

Binafsi namtetea Chasambi, lilikuwa ni kosa la kimpira kama ambavyo makosa mengine yanatokea, hivyo wanachama na mashabiki wa Simba wanapaswa kumsamehe na kutomwekea kinyongo moyoni. Najua wameumia kwa watani zao wa jadi kukaa kileleni nao kushuka, huku aliyefanya hivyo ni winga huyo ambaye amefunga bao ambalo lingeweza kuepukika kama angetulia tu na mpira. Kama alivyosema Kocha Mkuu, Fadlu Davids, bado ni kijana mdogo watu wasimsakame sana, watamharibia maisha yake ya soka.

Baada ya kumtetea, napenda kumpa ushauri wa bure Chasambi, ajue anacheza klabu kubwa na si Mtibwa Sugar. Klabu za Simba, Yanga au hata Azam, siyo za kufanya makosa yanayoweza kuzuilika.

Timu hizi zina mahitaji makubwa na aina ya wachezaji inayotaka kuwa nao, hivyo aepuke kufanya makosa kama hayo tena.

Mfano, sikuona haja ya kurudisha mpira nyuma, tena akiwa pembeni mwa uwanja, ambapo angeweza kupasua na kwenda mbele. Kingine anajua tabia ya kipa wake Camara, huwa mara nyingi anasogea mbele, hasa kama timu inashambulia, hivyo alipaswa kujua kwa muda ule hatokuwa langoni, na hatokuwa amejiandaa kupokea pasi ndefu na ya ghafla kiasi kile.

Nimwambie tu Chasambi timu kubwa kukosea kwa aina ile ni mwiko, huko nyuma kuna wachezaji walifanya hivyo na ikawa mwisho wa maisha yao kwenye 'karia' ya soka kwenye klabu hizo, au soka lenyewe kwa ujumla.

Moja ya sifa ya mchezaji wa timu kubwa ni kujua nini cha kufanya wakati gani na muda sahihi, pia kuepuka kufanya makosa ya aina ile.

Najua kwa sasa wanapitia kwenye wakati mgumu, yatapita, lakini namkumbusha tena kuwa tayari ana 'risiti' ya wanachama na mashabiki wa Simba, awe makini, chochote atakachokifanya ambacho sicho cha kawaida baadaye inaweza kumgharimu.

# Waziri azinyoshea kidole halmashauri

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohammed Mchengerwa, amewataka wakurugenzi wa halmashauri nchini, kukamilisha miradi yote ambayo tayari fedha zake zimetolewa na serikali.

Mchengerwa alisema hayo juzi jijini hapa, wakati akifunga kikao kazi kuhusu mfumo wa kielektroniki wa ununuzi wa umma (NeST) kilichoandaliwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA).

Alisema hivi sasa kuna mamlaka nyingi za serikali za mitaa ambazo bado hazijakamalisha miradi ambayo tayari fedha zilishatolewa na serikali hali ambayo inawanyima wananchi fursa ya kutumia huduma hizo.

"Kuna halmashauri ambazo bado majengo ya shule au vituo vya afya hayajakamilika lakini serikali tayari ilishamaliza kutoa fedha. Niwaagize wakurugenzi wote kumaliza miradi hiyo ili kutoa fursa kwa wananchi kuzitumia huduma hizo.

"Mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi mnapaswa kwenda kukamilisha miradi yote ya serikali ambayo mmepewa katika maeneo yenu. Kila mmoja wetu apunguze hoja na changamoto ambazo tunaweza kuzimaliza," alisisitiza.

Kuhusu mfumo huo wa NeST, aliiagiza PPRA kuweka program maalum ya kutoa mafunzo kwa watumiaji ili kupunguza malalamiko ambayo yamekuwa yakitolewa katika maeneo mbalimbali nchini.

"PPRA mnapaswa kuandaa programu za mafunzo kwa walaji ili kusaidia kujibu changamoto mbalimbali mbazo zimekuwa zikijitokeza kuhusu mfumo huu wa udhibiti wa ununuzi wa umma," alisema.

Pia alisema katika utelezaji wa mfumo huo kumekuwepo na changamoto mbalimbali ikiwemo baadhi ya mamlaka za serikali za mitaa kutoutumia na kukiuka takwa la kisheria.

Alisema changamoto nyingine ni halmashauri kutotenga asilimia 30 ya bajeti ya ununuzi kwa ajili ya makundi maalum wakiwamo wenye ulemavu, vijana na wanawake.

"Taasisi zote za ununuzi wa umma kwa mujibu wa sheria zinapaswa kutenga asilimia 30 ya bajeti ya ununuzi wa umma kwa ajili ya makundi maalum, hivyo nizitake taasisi zote za umma kutekeleza takwa hilo la kisheria," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa PPRA, Denis Simba, alisema kikao kazi hicho lengo lake ni kutoa mafunzo kuhusu mfumo wa NeST, kwa wabunge,wakurugenzi wa halmashauri na makatibu tawala wasaidizi.

# Mapunjo aipongeza PSSSF uendeshaji mikutano kidigiti

**Na Joseph Mwendapole**

MENEJIMENTI ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), imepongezwa kwa kuanzisha mfumo wa kuendesha vikao vyake kidigiti.

Pongezi hizo zilitolewa jana na Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya Mfuko huo, Joyce Mapunjo, wakati akizindua mfumo wa kuendesha vikao vya Baraza la Wafanyakazi pasipo kutumia karatasi.

Uzinduzi huo ulifanyika katika siku ya kwanza ya mkutano wa siku mbili wa Baraza la Wafanyakazi wa PSSSF, unaofanyika katika Manispaa ya Singida.

Akizungumza katika uzinduzi huo, Mapunjo alisema hatua ya kuachana na matumizi ya makaratasi katika kuendesha vikao vya baraza inaokoa fedha, kuongeza tija na ufanisi.

Alimpongeza Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, Abdul-Razaq Badru kwa mafanikio ambayo imeyapata kwa kipindi cha mwaka uliopita, ikiwa ni pamoja na kuboresha huduma kwa wanachama na wastaafu na kuongeza mapato ya uwekezaji.

Alisema maboresho hayo yamesababisha kuongezeka kwa uhimilivu wa mfuko huo, hivyo kuenda sanjari na maono ya Rais Samia Suluhu Hassan.

"Kwa mafanikio mliyopata inaonesha kuwa kuna vitu mnaweza mkafanya mkawa mfano bora katika nchi hii na kwa hakika kabisa kwa ufanisi mnaoonesha, mimi ninafurahi sana kufanya kazi na nyie.

"Ninashukuru kufanya kazi na nyinyi, ninaomba tushirikiane vizuri ili tufanye kazi nzuri hadi watu tunao wahudumia waseme PSSSF is the best," ni taasisi bora zaidi," alisema Mapunjo.

Alisema pindi bodi yake itakapoteuliwa, anaahidi kushirikiana na wajumbe wake, Mkurugenzi Mkuu na wafanyakazi wote wa PSSSF ili kufanyakazi kwa bidii na maarifa kuufanya mfuko huo kufikia matarajio ya Rais Samia pamoja na wadau wote katika sekta ya hifadhi ya jamii.

Wakili Peres Janathan Kageze, ambaye ni Mwakilishi wa Muungano wa vyama vya Wafanyakazi (TUICO) Taifa, anayesimamia sekta ya fedha, aliipongeza PSSSF kwa kuzidi kuimarisha uhimilivu wa mfuko.

Alisema uhimilivu huo awali ulikuwa asilimia 20, lakini kutokana na kazi kubwa inayofanyika hadi mwaka jana umeongezeka hadi asilimia 36.4.

"Ninawapongeza PSSSF kwa utendaji wao katika kutoa huduma bora, lakini pia pamoja na jitihada za kuboresha maslahi ya wafanyakazi.

"Sisi chama cha wafanyakazi tunaipongeza PSSSF kwa hatua hiyo muhimu na tunatoa wito kwa taasisi nyingine pia kuiga mfano huo," alisema.

Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi (PSSSF), Badru alisema kuwa baraza la wafanyakazi ni kiungo muhimu kati ya menejimenti na wawakilishi wa wafanyakazi, liko kisheria na ina katiba yake.

Alisema katika mkutano huo, watawasilisha malengo na mikakati ya baraza kwa mwaka wa fedha wa 2024/25 na kufanya tathmini ya utekelezaji wa mipango hiyo. Alisema pia watajadili changamoto na namna ya kuzitatua ili kuongeza ari, tija na kuongeza ufanisi.

Badru alisema mafanikio makubwa yaliyopatikana katika miezi 12 iliyopita, yanatokana na kuiishi Falsafa ya 4R za Dk. Samia, husunani zile mbili za mageuzi na kujenga upya.

"Ndio maana tathmini iliyofanywa mwaka jana imeonesha uhimilivu wa mfuko wetu umeongezeka kutoka asilimia 20 mwaka 2020 hadi asilimia 36.4 mwezi Juni, 2024, mapato ya uwekezaji yameongezeka," alisema Badru.

Badru alishukuru kwa ushirikiano aliopewa na wafanyakazi wenzake ndani ya miezi 12 akiwa Mkurugenzi Mkuu wa mfuko huo.

Alisema siri ya mafanikio ya mfuko ni mabadiliko ya utamaduni wa kazi, elimu ya hifadhi ya jamii kwa wanachama, kuongeza mafao ya wastaafu na uwekezaji kwa wanachama.

Alitaja mambo mengine kuwa ni pamoja na bidii ya kazi, ubunifu katika huduma na miradi ya uwekezaji na kufikia safari ya kuyafikia maono ya Rais, Samia na mchango mahsusi wa PSSSF kwa taifa.

Alisema thamani ya mfuko imekua kufikia Sh. trilioni 10 hadi mwezi Juni 2024, wakati mapato uwekezaji yamekuwa kufikia Sh. bilioni 800 kutoka Sh. bilioni 600.

Badru ambaye aliwahi kufanya kazi katika Benki ya Dunia (WB) alisema upangishaji wa majengo ya PSSSF umeongezeka na hadi Juni 2024, ulikuwa hadi asilimia 99 kwa nyumba za kuishi na asilimia 79 kwa nyumba za biashara.

Wafanyakazi wawili wa PSSSF, Amina Kassim na Abdallah Adam, walipewa zawadi ya cheti kwa kuibuka wafanyakazi bora kwa mwaka huu.



Polisi Kata ya Kisangura, Wilaya ya Serengeti, mkoani Mara, Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, Geniune Kimario akizungumza baada ya kukabidhi kiti maalum kwa ajili ya mtoto mlemavu, Lucia Mwita (wa pili kulia), wilayani humo, juzi. Kulia ni Baba wa mtoto huyo, Mwita Nyamanyi. **PICHA: MPIGAPICHA**

# Mpango kituo forodha Kabanga kufanya kazi saa 24

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SERIKALI imesema inafanya jitihada ili Kituo cha Forodha cha Pamoja (OSBP) Kabanga, kinachotoa huduma kati ya Tanzania na Burundi, kufanya kazi kwa saa 24 ili kuongeza ufanisi.

Naibu Waziri wa Fedha, Hamad Hassan Chande, alisema hayo juzi alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Ngara, Ndaisaba Ruhoho, aliyetaka kujua mkakati wa serikali wa kuwezesha vituo vya forodha vya Murusagamba na Kabanga, kufanya kazi kwa saa 24.

Chande alisema kuwa Kituo cha Forodha cha Kabanga ni Kituo cha Pamoja (OSBP) cha kutoa huduma za forodha kati ya Tanzania na Burundi kina miundombinu wezeshi kama vile taa za ulinzi, vyombo vya ulinzi na usalama, na maeneo ya kukagulia bidhaa, wasafiri na wafanyakazi, hivyo kuwa na uwezo wa kufanya kazi saa 24 kwa upande wa Tanzania. "Ili kituo hicho kitoe huduma saa 24, upande wa Kobero nchini Burundi unapaswa pia kuwa tayari kutoa huduma hizo saa 24", alisema.

Chande alisema kwa sasa Kituo cha OSBP Kobero kwa upande wa Burundi kinatoa huduma kwa saa 12 tu, hivyo jitihada mbalimbali zinaendelea kufanyika ili kuwezesha mazingira ya kituo hicho kufanya kazi saa 24, hususan ulinzi na usalama.

Kuhusu kituo cha Murusagamba, Chande alisema hicho ni kidogo cha forodha kinachofanya kazi ya uzuiaji na hufanya kazi ya kuzuia magendo kwenye maeneo ambayo mwenendo wa bidhaa na watu ni mdogo.

Naibu Waziri Chande alisema kutokana na udogo wa mwenendo wa bidhaa na watu katika kituo cha Murusagamba, uwezekano wa kituo hiki kufanya kazi saa 24 kwa sasa haupo.

Akijibu maswali ya nyongeza kuhusu ufungaji wa kifaa cha ukaguzi eneo la Mutukula lililoko mpaka wa Tanzania na Uganda na Kituo cha Horohoro, Tanga kati ya Tanzania na Kenya, Chande alisema kwa upande wa Mutukula tayari mkandarasi yuko eneo la mradi kwa ajili ya kufunga kifaa hicho na upande wa Horohoro, serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inaangalia utekelezaji wake.

Pia alisema mazungumzo yanaendelea kuhusu uwezekano wa Kituo cha Forodha cha Malindi, Zanzibar kufanya kazi saa 24 kwa kuwa kwa sasa kinahudumia makontena 2,000 kwa mwezi licha ya kufanya kazi kwa saa 12.

Alisema serikali inaendelea na mazungumzo na upande wa Zanzibar na kwamba kukamilika kwa mazungumzo hayo kutawezesha huduma hiyo.

# Rasimu ya kuondoa tozo zisizo rafiki migodini yaja

**Na Jenifer Gilla**

SERIKALI imesema kuwa ipo mbioni kutoa rasimu zitakazosaidia kumaliza changamoto ya tozo isiyo rafiki inayolalamikiwa na wachimbaji wadogo.

Hayo yalisemwa jana bungeni na Waziri wa Madini, Anthony Mavunde, wakati akijibu swali la Mbunge wa Busanda, Tumaini Magessa, aliyehoji ni lini serikali itapitia upya tozo zilizoko kwenye mnyororo wa uchimbaji na uchenjuaji wa dhahabu zinazowaelemea wachimbaji wadogo.

Akijibu swali hilo, Waziri Mavunde alisema rasimu ya mapendekezo ya maboresho ya tozo tayari imeshaandaliwa na ipo katika hatua ya kufanyiwa mapitio, ambapo matokeo yake yatasaidia kupanga tozo rafiki kwa wachimbaji wadogo.

"Rasimu hiyo ipo katika ngazi ya mapitio kwa makatibu wakuu na baada ya hapo itawasilishwa ili itolewe uamuzi," alisema.

Alisema awali wizara kupitia Mkakati wa Kuboresha Mazingira ya Biashara nchini (MKUMBI) ilifanya utafiti wa tozo 66 zinazotozwa na halmashauri katika shughuli za madini yakiwamo madini ya dhahabu.

Alisema tozo zilizobainika katika shughuli za uchimbaji na uchenjuaji wa dhahabu ni pamoja na ushuru wa karasha, ada ya ukaguzi, "Vat leaching, mialo, ushuru wa kusafirisha mi-amba ya madini na mabaki ya miamba baada ya kuchenjuliwa.

Alisema katika kutatua changamoto hizi, mwezi Agosti, mwaka jana, wizara iliitisha kikao Mkoa wa Singida ambacho kilishirikisha Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI). Kadhalika alisema ilishiriki Wizara ya Fedha, Tume ya Madini, STAMICO, Halmashauri za Wilaya (Ikungi, Chunya, Kahama, Msalala, Meatu, Shinyanga, Mtama na Lindi), FEMATA na TAWOMA.

Alisema kutokana na changamoto za kikodi, Rais Samia Suluhu Hassan aliunda Tume ya Maboresho ya Kodi ili ifanye tathmini ya mfumo wa kodi na kuleta mapendekezo ya namna ya kuboresha mfumo wa kodi.

"Ni imani yetu kuwa maboresho hayo yataangazia changamoto za kikodi zinazoikabili sekta ya madini," alisema.

Waziri Mavunde alisema serikali ilitunga kanuni ambayo inamtaka mwenye leseni na mwenye maduara waingie makubaliano ili kuepusha migogoro baina ya wamiliki wa migodi na wachimbaji wadogo.

Alisema sheria inaelekeza kuwa kila anayepewa leseni achimbe yeye na si kupangisha, hivyo mmiliki akikubali kuingiza mchimbaji mdogo ni lazima waingie makubaliano.



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea, mkoani Lindi, Adinan Mpyagila (kushoto), akikabidhi funguo ya pikipiki ya magurudumu matatu kwa mjasiriamali Mfaume Ng'ombo aliyopewa na Halmashauri ya Nachingwea kutokana na mkopo wa asilimia 10 mapema wiki hii. Kulia ni Mkuu wa wilaya hiyo, Mohamed Moyo. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# MOI yaanza upasuaji wa mgongo kwa matundu

**Na Joseph Mwendapole**

TAASISI ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI), imeanza rasmi kutoa huduma mpya za upasuaji uti wa mgongo kwa kutumia matundu (spine endoscope).

Kuanza kutolewa kwa huduma hiyo, kutasaidia ufanisi wa upasuaji huo na kuwezesha wagonjwa kukaa siku chache wodini.

Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk Mpoki Ulisubisya, alisema juzi jijini Dar es Salaam wakati wa kambi maalum ya matibabu ya kibingwa ya uti wa mgongo kwa njia ya matundu ambapo wagonjwa 12 watafanyiwa upasuaji.

Alisema MOI inakuwa taasisi ya kwanza nchini kutoa huduma hizo baada ya kupokea mashine ya kisasa (endoscope tower) ya kufanyia upasuaji huo yenye thamani ya Sh. milioni 500 kutoka kampuni ya Joimax ya Ujerumani.

Dk. Ulisubisya alisema mashine hiyo inaifanya MOI kuwa kinara katika utoaji wa huduma za upasuaji wa uti wa mgongo kwa matundu katika ukanda wa Afrika Mashariki, Kati na Kusini na kuchagiza dhana ya tiba utalii. "MOI imekuwa taasisi ya kwanza katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati kuwa na kifaa hiki cha kisasa kitaongeza ufanisi wa upasuaji na wagonjwa watapona kwa haraka na kupunguza muda wa kukaa wodini," alisema.

Mkurugenzi wa Huduma za Upasuaji wa Ubongo na Uti wa Mgongo, Dk. Lemeri Mchome, alisema huduma hiyo itasaidia wagonjwa kupata nafuu kwa haraka kutokana na kupata jeraha dogo wakati wa upasuaji.

"Awali MOI ilikuwa ikifanya upasuaji kwa kufungua eneo kubwa hivyo kumlazimu mgonjwa kukaa muda mrefu wodini akiuguza jeraha na kumuacha na kovu kubwa.

Mfano mgonjwa alikuwa analazwa siku tano au zaidi baada ya upasuaji kutokana na ukubwa wa jeraha, pia maumivu kwa mgonjwa yalikuwa makali, lakini kwa kutumia mashine hii changamoto hizo zote zitakuwa zimeisha, " alisema Dk Lemeri

Naye Mkufunzi wa Mafunzo kutoka Chuo Kikuu cha Tiba cha Weill Cornel cha Marekani, Dk Osama Nazar Kashlan, alipongeza MOI kwa kuwa tayari kuwekeza katika ujuzi wa watumishi wake. Aliahidi kuendelea kuwajengea uwezo watumishi wa taasisi hiyo katika huduma za kibingwa na kibobezi ili waendane na mabadiliko ya teknolojia duniani.

# Waridhishwa utendaji wa mahakama kidigitali

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WANANCHI mkoani Morogoro wameridhishwa na utekelezaji wa utoaji huduma za mahakama kwa mfumo wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Wamesema mfumo huo unarahisisha upatikanaji wa huduma za mahakama na kuwapunguzia gharama zikiwamo za nauli za kutoka sehemu moja kwenda nyingine kupata huduma.

Kauli hiyo imetolewa baada ya Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Prof. Elisante Ole Gabriel, kuzungumza na vyombo vya habari kuhusu utekelezaji wa bajeti ya mahakama na majukumu kwa nusu ya mwaka wa fedha 2024/25.

Mkutano huo uliofanyika kwenye kituo cha jumuishi cha utoaji haki cha Mahakama Kuu Kanda ya Morogoro.

Mkazi wa Kata ya Kihonda, Manispaa ya Morogoro, Janeth Sheiza, alisema utekelezaji huo ukiwamo mahakama inayotembea, umesaidia kukamilisha mashauri yote kwa haki na upatikanaji wa haki stahiki kwa umma.

Ivan Calvin, msaidizi wa mawakili wa kujitegemea alisema, maboresho hayo ya mahakama yametoa hamasa ya ufanyaji kazi na kuwapo kwa huduma za kidigitali kumesaidia kuepusha gharama na upatikanaji huduma kwa haraka.

Prof. Ole Gabriel alisema tayari mashauri 2000 yamesikilizwa na kumalizika ambayo ni sawa na asilimia 98.5 ya mashauri yaliyoka katika mahakama kwa sasa.

Alisema utekelezaji wa vituo hivyo sita vilivyoko kwa sasa, umeleta hamasa ya kufanya Benki ya Dunia (WB) kuridhika na ufanisi huo na kuwaongezea awamu nyingine ya fedha Dola za Kimarekani milioni 90, ambazo ni sawa na Sh. bilioni 207.

Prof. Ole Gabriel alisema kupatikana kwa fedha hizo kutasaidia kuongeza idadi ya vituo jumuishi vinavyojengwa katika mikoa ya Katavi, Simiyu, Songwe, Ruvuma, Geita, Lindi, Njombe, Singida na Pemba.

Alisema kwa sasa wameweka nguvu kubwa katika mahakama za mwanzo hasa katika utoaji wa huduma wa mahakama inayotembea kwenye wilaya kubwa kama vile ilivyo Wilaya ya Sikonge.

Alisema hadi sasa Mahakama ya Tanzania imevuka lengo la asilimia 100 ya utekelezaji wa huduma za mahakama na umaliziaji wa mashauri.





# Mabilioni kujenga miradi ya umwagiliaji Singida

**Na Thobias Mwanakatwe,** IRAMBA

SERIKALI imetoa Sh. bilioni 80.9 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kilimo cha umwagiliaji cha mazao mbalimbali katika Mkoa wa Singida.

Mhandisi wa Umwagiliaji wa Mkoa huo, Japhet Senyinah, alisema hayo juzi wakati wa hafla ya kukabidhi mradi wa upimaji na uchimbaji visima vya maji iliyofanyika Kijiji cha Kyalonsangi Kata ya Kinampanda wilayani hapa.

Senyinah, alisema utekelezaji wa miradi ya uchimbaji visima hivyo ni njia mojawapo ya kuongeza uhakika wa kupata chakula cha kutosha na kuwawezesha wananchi kutumia sekta ya kilimo kujikomboa kiuchumi.

Alisema katika mkoa huo kuna miradi ya umwagiliaji mitano yenye thamani ya Sh. bilioni 80.922, itakapokamilika itawanufaisha wakulima 7,500 na kuongeza eneo la kilimo cha umwagiliaji hadi kufikia hekta 15,000.

"Mkoa wa Singida tumeletewa miradi mitano ya umwagiliaji ambayo ni pamoja na Mradi wa Msingi wenye thamani ya Sh. bilioni 34.176 uliopo wilayani Iramba, mwingine wa Msange, Singida ambao una thamani ya Sh.bilioni 17.75, " alisema.

Senyinah, alisema hivi karibuni atakabidhiwa mkandarasi mradi wa Bwasa uliopo wilayani Manyoni wenye thamani ya Sh. bilioni 18.5 kwa ajili ya kuanza ujenzi.

Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Suleiman Mwenda, akizungumza katika hafla hiyo, alisema serikali inajenga miradi hiyo kwa lengo la kuwakomboa wananchi na umaskini.

"Tunapoboresha kilimo cha umwagiliaji na kukifanya kiwe cha kisasa na chenye tija kitawawezesha wananchi kujikwamua na umaskini kwa sababu watapata fursa ya kulima mara mbili zaidi kwa kila msimu na kupata mazao ambayo watauza," alisema Mwenda.

# Katibu Mkuu TAMISEMI, Mtendaji Mkuu TARURA wabanwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Adolf Ndunguru ameagizwa kukamilisha kuandaa Muswada wa Sheria kwa ajili ya Usimamizi na Uendelezaji wa Makao Makuu Dodoma ili upelekwe kabla ya Bunge la 12 kuvunjwa mwaka huu.

Vilevile, Katibu Mkuu huyo ameagizwa na Mtendaji Mkuu Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) kufanya tathmini ya makandarasi ambao hawajakamilisha miradi hadi Februari mwaka huu ili kuwafungia wasipewe kazi yoyote akiwamo anayejenga barabara za Jiji la Dodoma.

Maagizo yaliyatolewa jana na Waziri wa TAMISEMI, Mohamed Mchengerwa katika hafla ya utiaji saini mkataba wa ujenzi wa Soko Kuu la Majengo na vituo vya daladala vya jiji hilo kupitia Mradi wa Uboreshaji Miundombinu ya Miji (TACTIC) awamu pili chini TARURA.

Akizungumza katika hafla hiyo jana jijini hapa, Mchengerwa, alisema Rais Samia Suluhu Hassan aliagiza kuwa na sheria hiyo, hivyo haiwezekani kuwa na makao makuu kwa matamko pekee.

Alisema ni lazima kuwa na sheria ili asiwepo Mtanzania yeyote atakayekuja kubadilisha hilo.

"Sheria hii iharakishwe kama zinavyoharakishwa nyingine ili iingie bungeni kabla ya kuvunjwa kwa Bunge hili. Tutamuomba mheshimiwa Rais kwa hati ya dharura," alisema. Kuhusu utekelezaji wa barabara za jiji hilo, Mchengerwa, alisema serikali imetoa fedha na tayari makandarasi wamelipwa, lakini hadi sasa wapo chini ya asilimia 50.

"Haiwezekani serikali kutoa fedha Sh. bilioni 24, halafu wapo wanaorudisha nyuma jitihada za Rais Samia. Iwe kampuni ya Kitanzania ama ya kigeni wasiruhusiwe kupewa kazi hadi pale miradi yote iwe imekamilika," alisema.

Vilevile, Mchengerwa alipokea maombi ya Mbunge wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, kuhusu kujengewa kipande cha urefu wa kilometa 1.8 cha barabara ya Iringa Road hadi Michese na ya mita 750 eneo la Madukani.

**"Rais hawezi kutuelewa, ameleta fedha nyinyi, wajibu wenu kuweka utaratibu mzuri ili waweze kupata njia nzuri ya kuingia stesheni pale," alisema na kusisitia kuwa:**

Aliwaagiza TARURA kuwa ombi hilo ndicho kipaumbele namba moja katika ujenzi wa barabara za jiji hilo na kuonya haiwezekani Dodoma iwe makao makuu lakini ina barabara za changarawe.

Akizungumzia kero ya uingiaji na utokaji wa abiria katika kituo cha treni cha Reli ya Kisasa (SGR), aliwaagiza Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mkurugenzi wa jiji hilo na Mkuu wa wilaya kukutana na Shirika la Reli Tanzania (TRC) kuweka utaratibu mzuri.

"Rais hawezi kutuelewa, ameleta fedha nyinyi, wajibu wenu kuweka utaratibu mzuri ili waweze kupata njia nzuri ya kuingia stesheni pale," alisema na kusisitia kuwa:

"Nawataka nyie na TARURA, kazungumzeni na Wizara ya Uchukuzi, muweke utaratibu wa Watanzania wanaoingia na kutoka Dodoma waweze kuingia na kupita vizuri eneo hilo," alisema.

Waziri huyo, aliwataka watendaji hao ndani ya wiki moja wamwandikie jinsi watakavyotekeleza agizo hilo.

Awali Mtendaji Mkuu wa TARURA, Victor Seif, alisema awamu ya pili ya mradi huo katika jiji hilo inahusisha ujenzi wa vituo vya mabasi, daladala, uboreshaji wa soko hilo la Majengo na vivuko.

Seif, alisema miradi hiyo inayotekelezwa kwa miezi 12 chini ya Mradi wa Kuboresha Miji 45 (TACTIC) ina thamani ya Sh. bilioni 14.2.

Kwa upande wake, Mavunde ambaye pia ni Waziri wa Madini, alisema mradi huo ukikamilika, utatua kero ya wafanyabiashara na wanafunzi wa mitaa ya Mailimbili na Sechelela.

Alisema kukamilika kwake, kutaondoa kero ya wanafunzi hao kushindwa kwenda shule kutokana na korongo kujaa maji wakati mvua zinaponyesha.

"Watoto wanaoishi upande wa pili (wa Mailimbili) wamekuwa wakishindwa kuvuka korongo kwenda upande wa pili kwa sababu hakuna namna ya kufanya hadi kuzunguka umbali mrefu sana. Na hivyo wanashindwa kwenda shule," alisema.




Mwandishi wa habari wa gazeti la Nipashe, Mkoa wa Singida, Thobias Mwanakatwe (kushoto), akipokea tuzo kutoka kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa), Mohamed Mchengerwa, mjini Singida juzi, zilizotolewa na Mradi wa Shule Bora, baada ya kuibuka mshindi wa kuandika habari kuhusu masuala ya elimu, mkoani humo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watakiwa kujitambulisha mfumo anwani za makazi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Jerry Slaa, amesema asilimia 95 ya maeneo nchini yameingizwa katika mfumo wa anwani za makazi na kuwahimza wananchi kujitambulisha, kuwasilisha changamoto zao na kupatiwa ufumbuzi.

Silaa aliyasema hayo juzi wakati akifungua Maadhimisho ya Wiki ya Anwani za Makazi yanayofanyika jijini hapa.

Slaa, alisema mpango wa serikali ilikuwa ni kuitambua nchi yote na hilo linakwenda kutimia hadi kufikia mwaka 2022, asilimia 95 ilikuwa imeingizwa kwenye mfumo huo.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan, alielekeza utekelezaji wa operesheni ufanyike kwa miezi minne kuanzia Februari hadi Mei mwaka 2022.

Alisema uratibu huo, ulifanyika chini ya usimamizi wa wakuu wa mikoa, Mei 31, mwaka huo, utekelezaji wake ulikamilika kwa mafanikio makubwa.

Silaa, alisema zaidi ya taarifa milioni 12.3 za anwani za makazi zilikusanywa kwa kipindi hicho na kuhifadhiwa katika mfumo huo wa kidijitali wa anwani za makazi uitwao NaPA.

Aliwataka wananchi kuzitumia anwani za makazi kwa ajili ya kujitambulisha maeneo walipo, kuwasilisha changamoto na kufikiwa na watendaji wa mitaa, vijiji na waratibu wa halmashauri nchini.

Slaa, alisema dhamira ya serikali ni kuhakikisha kila nyumba, jengo, kiwanja, huduma, ofisi na eneo la biashara vinatambulika kwa anwani ya makazi.

Alisema nchini, mgawanyo wa anwani hizo umefanyika katika ngazi ya kata, kila moja ikiwa na namba yake yenye tarakimu tano kurahisisha utoaji na upokeaji wa huduma ili kuchochea maendeleo ya uchumi na jamii.

Kwa mujibu wa Silaa, mfumo umeanza kutumiwa na baadhi ya wananchi na taasisi na manufaa kuonekana kutokana na huduma mbalimbali kutolewa.

Alizitaja baadhi ya huduma hizo kuwa ni barua ya utambulisho ya kidijitali na mahali elimu inaendelea kutolewa.

Alisema utekelezaji wa mfumo huo ni endelevu kwa sababu ya mabadiliko ya makazi, wakazi, huduma, kukusanya, kuhakiki na kuhuisha taarifa.

Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Festo Dugange, alisema wizara hiyo imeanza kutumia mfumo huo kwa mitaa yote nchini kutambua makazi, huduma kwa wananchi kwenye sekta za afya, elimu na kufikiwa na wadau wengi.





# Shein atoa nasaha kwa viongozi CCM

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

ALIYEKUWA Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amewataka viongozi wa chama hicho kuendeleza historia ya visiwani hapa kwa manufaa ya vizazi vijavyo kujifunza historia iliyopo.

Dk. Shein, aliyasema hayo wakati akizungumza na viongozi wa Umoja wa Maskani za CCM Zanzibar (UMAZA) baada ya kwenda nyumbani kwake Kibele Wilaya ya Kati Unguja kumsalimia ikiwa ni sehemu ya sherehe ya kuzaliwa kwa chama hicho mwaka 1977.

Alisema historia ya Zanzibar ikitengenezwa vizuri, CCM kitaendelea kushinda siku hadi siku katika chaguzi zote nchini.

**"Katika kufanya kazi zenu muwe na lengo moja la umoja, msije mkagawika ili muweze kufanya jambo lilokuwa zuri na hata ushindi kuwa mkubwa wa CCM kwa asilimia kubwa,"**

Shein, aliutaka UMAZA kuendeleza umoja, mshikamano na maelewano ili kujenga fikra na kusaidia kuleta maendeleo nchini.

"Katika kufanya kazi zenu muwe na lengo moja la umoja, msije mkagawika ili muweze kufanya jambo lilokuwa zuri na hata ushindi kuwa mkubwa wa CCM kwa asilimia kubwa," alisema Shein.

Vilevile, alisema CCM ni chama kikubwa na kitaendelea kuongoza Tanzania endapo misingi iliyokuwapo itaendelezwa.

Katibu wa Maskani ya CCM Kisonge, John Mwakanjuki, alisema wataendeleza umoja wao na kuhakikisha ushindi unapatikana wa kishindo wa CCM katika Uchaguzi Mkuu utaofanyika nchini Oktoba mwaka huu.

Mwakanjuki, alisema umoja huo utaendelea kuwatembelea viongozi wakuu wastaafu ili kupata nasaha katika utendaji wao wa kazi.



Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Zanzibar, Abeida Rashid Abdallah, akitia saini mpango wa taifa wa kushughulikia utekelezaji wa Agenda ya Wanawake, kuhusu amani na usalama, ofisini kwake, Kinazini Unguja, mapema wiki hii. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# ZEC yakoshwa mwitikio wananchi daftari la wapigakura

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

TUME ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) imesema imeridhishwa na uandikishaji wa daftari la kudumu la wapigakura katika Wilaya ya Micheweni.

Hayo yalisemwa visiwani hapa na Makamu Mwenyekiti wa ZEC, Aziza Iddi Suwedi wakati akitoa taarifa kwa waandishi wa habari baada ya kuhitimishwa uandikishaji wa daftari hilo katika wilaya hiyo Jumatano wiki hii.

Aziza, alisema uandikishaji huo umefanyika kwa njia za demokrasia na kutoa nafasi kwa watu kujiandikisha bila ya kuwepo kwa mivutano.

Alisema mawakala wote wa vyama vya siasa waliruhusiwa kwenye mchakato wote katika vyumba vya uandikishaji.

Aliwataka wananchi kujitokeza kwa wingi katika Wilaya ya Mkoani ambako uandikishaji katika daftari hilo utaendelea.

"ZEC tumeridhishwa na zoezi la uandikishaji wa daftari la kudumu la wapigakura katika Wilaya ya Micheweni, tumeshuhudia watu wenye sifa kujiandikisha, mambo yote yakiwa wazi kabisa na kushuhudiwa na mawakala wa vyama vya siasa," alisema Aziza.

Mwakilishi wa Micheweni, Shaame Shamata Khamis, alisema uandikishaji katika daftari hilo umekwenda vizuri kwa watu wenye sifa kuandikishwa.

Khamis, aliwapongeza mawakala wa vyama vya siasa kwa kufuatilia uandikishaji huo bila ya kuibuka mivutano na kuweka pembeni ushabiki wa kisiasa.

"Mimi binafsi nimeridhishwa na uandikishaji wa daftari la wapigakura kwa wananchi wa Micheweni na shehia zake hatua ambayo matarajio yangu makubwa kuona Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu unafanyika katika misingi ya demokrasia," alisema.

Ali Hamad Hijja ni miongoni mwa wakala kutoka Chama cha ACT- Wazalendo, alisema uandikishaji unaendelea vizuri licha ya kuwapo kwa kasoro ndogo ikiwamo alama za vidole kushindwa kusoma vizuri kwenye mashine za kuandikisha wapigakura kielektroniki (BVR).

## Nchi za Afrika, Ulaya kushiriki maonesho nishati, umeme jadidifu

**Na Mwandishi Wetu**

NCHI nane za Afrika na Ulaya zinatarajia kushiriki maonesho ya kwanza ya teknolojia ya nguvu ya nishati na umeme jadidifu ili kuinua na kuongeza bunifu kwa wafanyabiashara nchini.

Akizungumza na vyombo vya habari, Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Nishati Jadidifu Tanzania (TAREA), Matthew Matimbwi, alisema maonesho hayo yanayofanyika kwa mara ya kwanza nchini, yameletwa kwa ushirikiano wa TAREA na Kampuni ya ETSIPL kutoka India.

Matimbwi, alizitaja nchi zinazoshiriki maonesho hayo ni mwenyeji Tanzania, Zambia, Falme za Kiarabu (UAE), Kenya, India, China, Afrika Kusini na Ujerumani.

Alisema maonesho hayo yana lengo la kukuza biashara ya teknolojia kwa wafanyabiashara wa Tanzania katika sekta ya nishati safi endelevu, masoko ya ndani na nje ya nchi, kujitangaza kimataifa na kuweka biashara kwenye viwango vya juu.

"Wafanyabiashara wa Tanzania watapata fursa kubwa sana kupitia maonesho haya kwani hapa kuna kampuni zaidi ya 100 kutoka nchi hizo nane ambao watabadilishana uzoefu na kukuza uwezo zaidi," alisema Matimbwi.

Alisema maonesho hayo yamelenga bidhaa kama vile nyaya, betri, taa, nishati mbunifu, elektroniki, usambazaji, uwekaji vifaa vya majumbani, UPS, mifumo ya majumbani, HVAC na mawasiliano ya simu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Chemba ya Wafanyabiashara wa Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA), Oscar Kissanga, alisema maonesho hayo yatawasaidia Watanzania kukuza masoko hasa kuelekea soko la Afrika la bidhaa za kilimo, madini na kuwafundisha kujitangaza zaidi.

Mmoja wa washiriki katika maonesho hayo, Nafsa Shabani kutoka kitabu maalumu cha kuweka anuani za kampuni (NCD), alifafanua kuwa kinasaidia kampuni za biashara, viwanda kuweka kumbukumbu na anuani zao.

Nafsa, alitaja faida nyingine ya kitabu hicho kuwa ni kuwezesha wapatikane kiurahisi katika kujitangaza kutafuta masoko ndani na nje ya nchi.

Alisema kitabu hicho kinatoka kwa mwaka kila mara mwezi Machi kwa kulipia gharama nafuu elekezi kwa anayehitaji.

Alisema kitabu hicho kinasambazwa kwenye hoteli zote ndani na nje ya nchi, balozi na viwanja vya ndege ili wahitaji waweze kufikiwa kwa urahisi.

P. DDDY
UKURASA 14





Nipashe
BT
BURUDANI TELE



# ABDUL KINGO

## BOSI ALIYEMPORA DIAMOND MREMBO WAKE

UKITAZAMA video ya wimbo mpya wa Diamond Platnumz, unaoitwa Nitafanyaje, macho yako yatakutana na bosi matata, ambaye anamwaga pesa kumteka mwanamke mrembo.

Mwanaume huyo ni Abdul Kingo, ambaye ameitendea haki nafasi yake kama 'Video King' kwenye video ya wimbo huo ambao kwa sasa unatamba.

Akizungumza na Nipashe, Kingo amesema imekuwa ni bahati kwake kushiriki kwenye video hiyo ya msanii huyo mkubwa Afrika na anachukulia kama historia katika maisha yake.

"Nilitamani siku moja nifanye kazi na msanii mkubwa hapa nchini, lakini sikujua kama Diamond Platnumz atakuja kutimiza ndoto hii. Namshukuru Mungu kwa hili ni jambo kubwa kwenye maisha yangu," amesema Kingo.

Kingo ambaye ana vipaji vingi ikiwamo uchoraji wa vibonzo na mwigizaji katika tamthilia mbalimbali, ameeleza kwamba ameshiriki katika video hiyo baada ya kushinda mchujo kutoka orodha ndefu ya wasanii.

Amesema Diamond alihusika kumchagua kuwa mhusika mkuu katika video ya wimbo huo.

"Maneno Juma ndiye aliyepeleka jina langu kwa Diamond, na baada ya kuchaguliwa nikawa katika mikono ya Hanscan kwa ajili ya uchukuaji picha katika maeneo tofauti ya Dar es Salaam," ameongeza kusema.

Aidha, amemwelezea Diamond ni mtu ambaye anajali kukuza vipaji vya wasanii, mwelekezaji na anayethamini kazi yake.

"Katika video ya wimbo mimi na yule mrembo tulifanya uhusika ulioshiba kwa sababu na Diamond ni mtu wa kazi zaidi haikuwa na ugumu wowote hadi tunamaliza," amesisitiza.

Kingo amesema wimbo huo umempatia mabadiliko katika fani yake ya uigizaji, baada ya kupokea madili mengi ya kazi pamoja na kuongezeka umaarufu wake.

"Matarajio yangu ni kufanya kazi zaidi na wasanii wakubwa wa ndani na mataifa mengine ya Kiafrika," amesema.

**BASI SAWA**

## Dogo Pepe ucheshi hadi baa



MCHEKESHAJI wa jukwaani, Dogo Pepe, amesema wasanii wengi fani hiyo wanatumia shoo za baa kama sehemu ya mazoezi.

Akizungumza na EATV, amesema wachekeshaji wengi wachanga wanatumia majukwaa ya aina hiyo kwa kujaribu kazi zao kabla ya kwenda kuonyesha maeneo mengine yanayotambulika.

"Unapofanya kazi kwenye baa au klabu ndogo kwa ajili ya kufanya mazoezi na kujaribu namna unavyokubalika na sio kupunguza thamani ya fani ya ucheshi kama inavyodaiwa na wengine," amesema Dogo Pepe.

## Cassypool amkejeli Willy Paul



MWANAMTANDAO maarufu nchini Kenya, Cassypool, amekejeli kolabo mbili zilizoachiliwa hivi karibuni na wasanii Bahati na Willy Paul, haziwezi kushindana na wanamuziki wa Tanzania.

Akizungumza na mtengenezaji wa maudhui Trudy Kitui, Cassypool alisema kwamba hakuna msanii wa Kenya anaweza faulu kama wanavyoimba wasanii hao wawili.

"Mimi nilisema huwezi kuimba kama Mbongo anavyoimba. Haiwezekani, unaimba kama Diamond na unataka utambe eti tunakusifia umetoa ngoma kubwa. Hiyo ni kuharibu wakati ni takataka." Alisema Cassypool.




# KEVIN CASH KILA KITU KWA MAMA

MWANAMUZIKI chipukizi, Kevin Cash, amesema mama yake anahusika na masuala yote ya pesa na hawezi kuingilia kuepusha migongano.

Amesema katika harakati zote za muziki mama yake amejitoa kutoa gharama ambazo zinamwezesha kukuza kipaji chake.

"Siwezi kuingilia suala la pesa, uongozi wangu ndio unajua suala hilo. Ninapoona nataka kufanya kitu mama ndiye ananisaidia na wakati wote namwambia anisaidie kama msanii na sio mtoto wake," amesema Kevin Cash.



# G Nako amtetea Diamond

RAPA mkali G Nako amesema dhana zinazojengwa na baadhi ya watu kuwa Diamond Platnumz, anapoteza wasanii wenzake kwa njia ya kishirikina sio sahihi na zinatakiwa kukemewa.

Akizungumza hivi karibuni, G Nako, amesema jina la Diamond limekuwa kubwa na hata baadhi ya wasanii waliofanya nao kazi walibebwa na umaarufu wake na sio kwamba nyota zao zimechukuliwa.

"Nyota zinachukuliwa vipi? Kama mtu umetoa wimbo wako kwa ukubwa ni lazima utakubalika, haya mambo hakuna kwani Diamond ni maarufu na hata ukifanya naye kazi lazima utabebwa na umaarufu wake na sio vingine," amesem G Nako.

**FILAMU**

# Barua ya jini, wino wa damu

**Na Adam Fungamwango**

NI filamu inayohusu vita kali ya kugombea mapenzi kati ya binadamu na jini. Inaitwa 'Barua ya Jini' ambayo imechezwa na waigizaji kina Ally Kizo aliyecheza kama Songoro, Jenifa Michael yeye ni Lina, Rachel Maulidi kama dada yake Songoro, Hanifa Said akicheza kama Asha, na wengineo walishiriki.

Majini ni moja kati ya viumbe vilivyoumbwa na Mwenyezi Mungu, lakini vikiwa na uwezo wa kujibadilisha kwa mwonekano wowote ule wanaoupenda.

Songoro na Lina ni wapenzi wanaopendana sana kiasi kutaka kuoana. Hata hivyo kuna siku Songoro anaopoa demu mmoja kwa namna ambayo hata yeye hajui amekubali vipi.

Baada ya siku chache anaokota bahasha, lakini ikiwa na ujumbe na pesa. Hata hivyo ujumbe huo ulioandikwa haueleweki vizuri, na anatokewa na mtu ghafla.

Mtu yule anamkumbuka kuwa ni yule demu. Akajitambulisha kwa jina la Asha na kumwambia yeye hakuwa binadamu wa kawaida bali ni jini.

Akamwambia alimpa mapenzi ya ajabu siku walivyokutana kiasi naomba awe wake peke yake na asiwe na mtu yoyote.

Kali kuliko yote akamkataza Songoro kuwa na uhusiano tena na Lina. Akamwambia kwa sababu yeye ni jini anaweza kujibadilisha na kuwa kama Lina au mwanamke yoyote yule mrembo duniani hata Beyonce, hivyo akitaka atakuwa anajibadilisha kuwa kama Lina.

Hiyo inamfanya Songoro kuwa na mawazo sana. Jini Asha anamtokea Lina na kumwambia aachane na mpenzi wake Songoro kwa sababu yeye anampenda sana.

Lina anafanya ubishi. Bado anakwenda kwa mpenzi wake Songoro. Kinachofanyika ni kwamba jini Asha anamgeuza Lina kuwa kipofu kwa dakika tano na baadaye anamfanya kuona. Anamwamboa hilo ni onyo, akirudia atamfanya kuwa kipofu daima. Lina akawa na woga, akawa haendi kwa Songoro.

Jini Asha na Lina wote sasa wakawa wajawazito. Mama yake Lina akaja kumwambia Songoro ni lazima amuoe binti yake kwa sababu ameshampa ujauzito. Jini Asha anamtokea Songoro na kumwambia ana mimba yake. Na ili awe salama kwa majini wenzake na wazazi wake ni lazima waoane. Songoro anakataa. Kwa hasira Asha anamgeuza taahira ambaye anashinda na kulala chini ya mti. Kila siku Asha anakuja na kumbembeleza waoane, pia akimtahadharisha kuwa kama akikataa, ataishi hivyo milele.





# BENDI ZILIZOITIA HOMA TWANGA PEPETA

**Na Adam Fungamwango**

Bendi ya African Stars 'Twanga Pepeta ilianzishwa mwishoni mwa mwanzoni mwa miaka ya 2000.

Ni baada ya kuibuka aina ya muziki ambao uliathiriwa na bendi za Congo DR kama Wenge Musica, Extra Musica ambazo zilifanya ziara nchini.

Aina ya upigaji wao na ziara za bendi hizo hapa nchini ulisababisha kuundwa kwa bendi moja iliyoitwa Diamond Sound wana Kibindankoi na baadaye Twanga Pepeta.

Baada ya kulitesa soko la muziki nchini, baadaye ziliundwa bendi zenye mlengo kama huo, ambazo zilipa ushindani mkubwa Twanga Pepeta na kunyang'anyana mashabiki na kuzua upinzani mkubwa kama wa Simba na Yanga.

**TOT Plus Band**

Ni bendi ya mwanzo kabisa iliyoanza kuitingisha Twanga Pepeta. Kwanza kabisa ilichofanya ni kumchukua kinara aliyekuwa kwenye kiwango cha hali ya juu na kipenzi cha bendi hiyo, Banza Stone.

Kujiunga kwa Banza kwenye bendi ya TOT kulisababisha upinzani mkubwa wa bendi hizi mbili na pia kuipaisha.

Pili ikawa maarufu na kuwa mshindani halisi wa Twanga Pepeta, kiasi cha kuvuta mashabiki wengi zinapopambana laivu au kupambanishwa kwenye redio na TV.

**Mchinga Sound Band**

Ilianzia mkoani Lindi, lakini ikaja kufanya makazi yake jijini Dar es Salaaam. Ni bendi ambayo nayo ilikuja kuisumbua mno Twanga Pepeta, kwa sababu iliwachukua baadhi ya wanamuziki wake kama Adolf Mbinga, Joseph Watugulu, Rogat Hega 'Katapila' na wengineo.

Hali hii ilisababisha mashabiki wa Twanga Pepeta kuiona si bendi rafiki kwao na kukawa na upinzani mkali si kati ya bendi hizo mbili tu, bali hata uongozi wa bendi hizo mbili nao mara kwa mara ulikuwa ukiingia kwenye mzozo.

**Chuchu Sound Band**

Kama kuna bendi ambayo ilikuja kwa kasi na kuondoka kwa kasi vile vile ni hii. Chuchu Sound ni bendi ndogo tu ambayo iliundwa na baadhi ya wanamuziki wa Kikongo na Kitanzania, lakini ilitesa na kuzoa mashabiki wengi kwa muda mfupi na kuziacha bendi nyingine, ikiwamo Twanga Pepeta zikiulizana.

Sababu ni staili yao. Ilikuja na aina mpya ya muziki ambao ulikuwa ni wa kimwambao maarufu kama 'mduara' uliokuwa ukihanikizwa na vionjo kutoka kwa wanamuziki kama Omari Mkali, Chuchu Yusuph mwenyewe, Mao Santiago, Jenico Flower na wengineo.

Ilipiga muziki wa aina zote, kama wa bendi za Twanga Pepeta, na mduara pia, lakini nyimbo za mduara ndizo zilioitambulisha zaidi bendi hiyo na kupendwa, Ikasababisha bendi nyingi, ikiwemo TOT kuanza kuiga nao kupiga mduara.

**FM Academia**

Baada ya kuipa changamoto Diamond Sound Band, wakati huo ikiitwa FM Musica, ilibadilisha jina na kujiita FM Academia. Sasa ikahamia kuipa wakati mgumu Twanga Pepeta, ikiwa na kina Nyosi El Sadaat. Ni bendi ambayo kwa kipindi kirefu imetoa ushindani mkubwa kwenye muziki wa dansi nchini hasa wa kizazi hicho kuanzia mwishoni mwa miaka ya '90 hadi leo.

**Stono Musica 'Wajelajela Original'**

Historia ya bendi hii haitofautiani na ya Chuchu Sound. Ilikuja kwa moto mkali, lakini ukazimika ghafla. Ilisumbua na kutesa, si kwa Twanga Pepeta tu, bali bendi zote na hasa FM Academia ambapo wanamuziki wengi walitoka huko.

Baadhi ya wanamuziki wa FA Academia raia wa Congo DR walikamatwa kwa kuishi nchini bila vibali.

Walikaa rumande kwa muda na baada ya kutoka walitunga wimbo wa 'Prison' au 'Chozi la Mnyonge,' lakini muda mfupi tu baadaye, walijiengua kwenye bendi yao na kuunda Stono Musica ambayo iliyotoa vibao kama 'Binadamu', 'Jimmy Chocolate,' 'Majivuno' na nyingine nyingi.

# Wizkid, Don Jazzy wayamaliza






MWANAMUZIKI wa Nigeria, Ayodeji Balogun, maarufu kama Wizkid, na mtayarishaji wa muziki Don Jazzy, wamethibitisha kumaliza ugomvi wao.

Wawili hao hivi karibuni wameonekana wakiwa pamoja na kuonyesha tofauti zao wamezimaliza.

Ugomvi kati ya wasanii hao ilianza wakati mwimbaji huyo wa ngoma ya Kese' alipoingia kwenye akaunti yake ya X na kuandika kwamba muziki wa Afro Beats umekufa.



## Portable anunua ugomvi

MWIMBAJI mwenye utata, Portable amejibu wimbo mpya wa msanii mwenzake Asake, akisema kingereza kilichotumika sio sahihi.

Wimbo huo wa Asake uliwalenga wale wanaomkosoa kuwa Kiingereza chake cha kuzungumza.


Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Portable, alimwambia mwanamuziki huyo kuwa ni kweli hawezi kuongea Kiingereza, hivyo upate mwalimu wa kumfundisha wakati bado ana pesa za kutosha.

## Kanye azidi kuwakera watu

PAMOJA na kulaumiwa kwa kitendo cha mke wake kuvaa vazi nusu utupu katika sherehe za tuzo za Grammy, rapa maarufu nchini Marekani, Kanye West amejigamba kuwa vazi hilo limekuwa bora zaidi kwa mwaka 2025.

Kanye aliandika kupitia ukurasa wake wa Instagram, kuwa mkewe Bianca, amepata umaarufu mkubwa kiasi cha kuwa kinara ya watu walioatafutwa kupitia mtandao wa google.

"Mtu aliyetafutwa zaidi katika google ni mwanamke aliyevaa vasi la YZY," aliandika, huku akijivunia vazi hilo ambalo liliwachukiza watu wengi.





## Diddy bado abanwa

MWANAMUZIKI maarufu wa Hip hop wa Marekani, Diddy, anayekabiliwa na kesi ya matumizi ya dawa za kulevya na unyanyasaji wa kingono, safari hii mwanamuziki wa kiume amejitokeza akilalamika kudhulumiwa na msanii huyo.

Kulingana na Jarida la Variety, mlalamikaji ambaye ni mwanamuziki mwenzake anayeitwa John Doe, aamewasilisha malalamiko hayo kortini kupitia wakili wake Tony Buzbee.

Buzbee alidai kuwa John Doe alikuwa na matamanio ya kuingia kwenye tasnia ya muziki kama rapa na mwimbaji mwaka wa 2015, alipewa kinywaji chenye kulevya na kisha kumnyanyasa kingono wakati alipomfuata klabu ya usiku kumuomba amsajili kwenye lebo yake.

## Martin atua Kenya kutoa burudani

Mwanamuziki wa Reggae kutoka Jamaika Chris Martin, amewasili nchini Kenya kwa ajili ya kuburudisha tamasha la Sauti Kutoka Afrika, linalofanyika leo.

Msanii huyo atakuwa mara yake ya tatu kutoa burudani kwa mashabiki wa muziki huo nchini Kenya, mara ya kwanza ilikuwa 2010.

"Nina furaha kurudi Kenya tena. Nilikuja hapa kwa mara ya kwanza miaka 15 iliyopita na Wakenya hawajanionyesha kitu chochote zaidi ya upendo," alisema Chris Martin.





# Polisi kuweka hadharani kilichoua watatu kwa kunywa pombe kali

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

JESHI la Polisi Mkoa wa Manyara, linatarajia kutangaza hadharani muda wowote ripoti yake ya uchunguzi kuhusu vifo vya watu watatu, waliopoteza maisha kwa kunywa pombe kali.

Tayari, jeshi hilo limeruhusu familia za marehemu, kuchukua miili ya wapendwa wao na kwenda kufanya maziko.

Akizungumza jana na Nipashe kwa njia ya simu, Kamanda wa Polisi wa Mkoa huo, Ahmed Makarani, alisema muda wowote kuanzia sasa watatoa ripoti hiyo ya uchunguzi.

Watu hao waliopoteza maisha wiki iliyopita baada ya kunywa pombe kali katika Kijiji cha Bashnet, Wilaya ya Babati.

"Uchunguzi bado, kwa kuwa mambo haya yalitokea mwishoni mwa wiki iliyopita na sampuli tulizipeleka kwa Mkemia wa Serikali Jumatatu ya Februari 3, mwaka huu, ila tunategemea majibu yake muda wowote na tutaita vyombo vya habari na kuwapa taarifa," alisema Makarani.

**"Sisi tulishapeleka sampuli hizo kwa mtaalamu wa MMS (Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali), kwa ajili ya uchunguzi, atakuja kuonyesha kitu gani amekiona, baada ya tukio,"**

"Sisi tulishapeleka sampuli hizo kwa mtaalamu wa MMS (Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali), kwa ajili ya uchunguzi, atakuja kuonyesha kitu gani amekiona, baada ya tukio," alifafanua.

Alisema ili kudhibiti unywaji pombe mpaka kusababisha mauti, ni vizuri watu wawe na kiasi, wakinywa wasinywe kupitiliza kama ambavyo matangazo ya wauzaji yanavyoelekeza.

Alipoulizwa na Nipashe namna gani watadhibiti uuzaji wa pombe kali za moshi aina ya gongo ukanda wa Bashnet, alisema wanafanya doria ili kuwanasa wauzaji.

Mkazi wa Babati, Anna John, alisema wananchi wana hamu na taarifa ya uchunguzi ili wajue ni kitu gani kiliua watu hao.



Baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Sekondari Ewong'on, Kijiji cha Kambi ya Chokaa, Kata ya Naisinyai, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, wakipanda miche ya miti kwa ajili ya kutunza mazingira ya eneo hilo, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# TAKUKURU yaokoa mamilioni kwa kuwaburuta kortini watumishi

**Na Oscar Assenga,** TANGA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imeokoa zaidi ya Sh. milioni 76.048 baada ya kuwafikisha mahakamani waliokuwa watumishi wa umma kwa tuhuma za ubadhirifu wa fedha za Wilaya za Kilindi, Korogwe na Tanga Jiji.

Mashtaka yanayowakabili ni kutowasilisha fedha hizo za serikali na kuzitumia kwa manufaa yao.

Fedha hizo zilikusanywa kwa mashine za kielektroniki za kukusanyia mapato (POS).

Jana Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Tanga, Ramadhani Ndwatah, alieleza hayo, wakati akitoa taarifa ya utendaji wa taasisi hiyo kwa kipindi cha Oktoba hadi Desemba mwaka jana.

Ndwatah, alisema baada ya kufikishwa mahakamani, Jamhuri ilishinda kesi hiyo na watumishi hao kuamriwa na kurejesha kiasi hicho fedha.

Alifafanua kuwa katika Wilaya ya Kilindi, Jamhuri imeshinda kesi za hujumu uchumi, namba 13 ya mwaka 2023, namba 11 ya mwaka 2023 na namba 06 ya mwaka jana dhidi ya watumishi hao.

"Kiasi cha shilingi 58,678,780.00 zilirejeshwa na watumishi hao, kwa amri ya mahakama sambamba na adhabu nyingine," alisema.

Alisema wilayani Korogwe Sh. 9,198,045.31 zilirejeshwa kwa amri ya mahakama baada ya Jamhuri kushinda kesi za uhujumu uchumi, namba 09 ya mwaka 2023 na namba 10 ya mwaka 2023 dhidi ya washtakiwa hao.

"Katika Jiji la Tanga, Jamhuri ilishinda kesi za uhujumu uchumi namba 16,558 ya mwaka 2025 na namba 7 ya mwaka 2023. Shilingi 3,171,633.9 zilizofanyiwa ubadhirifu kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekta ya elimu, huku milioni tano zikiwa ni za mikopo ya asilimia 10, kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu," alisema Ndwatah.

# DC Hai, Same awatwisha majukumu

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

MKUU wa Wilaya Siha mkoani Kilimanjaro, Dk. Christopher Timbuka amewataka watumishi wa umma wilayani hapa kutekeleza majukumu kwa wananchi ili kutimiza kuzingatia sheria, kudumisha amani na utulivu katika jamii.

Dk. Timbuka alitoa wito huo wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya elimu ya uraia na utawala bora kwa watendaji wa ngazi ya vijiji na wilaya kwa ajili ya kwenda kuelimisha jamii.

Alisema watendaji hao wanapaswa kuwa mstari wa mbele kuielimisha jamii kwa sababu wako karibu nao na wanakutana nao mara kwa mara katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

"Naomba mkafanyie kazi mafunzo haya, msiende kubweteka na kuyaacha katika makaratasi na vitendea kazi mlivyotumia kuchukua mafunzo," alisema Timbuka.

Alisema serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria inatoa mafunzo hayo sehemu mbalimbali nchini kwa watendaji hao, hivyo wao kama watumishi, wanapaswa kuzingatia na kutelekeza kwa vitendo kwenye sehemu zao za kazi.

**KASILIDA MGENI**

Wakati huo huo, Mkuu wa Wilaya ya Same, Kasilida Mgeni, amewataka watendaji wilayani mwake kwenda kuleta mabadiliko kwenye maeneo yao ya kazi na kwa wananchi kwa kutumia mafunzo hayo kwa kuwa ni sehemu ya uboreshaji wa utendaji wa kazi.

"Tunashukuru Wizara ya Katiba na Sheria kwa kutoa mafunzo hayo, yanasaidia kuboresha utendaji kazi kwa watumishi wa umma," alisema Kasilida wakati wa mafunzo kwa watendaji hao wilayani humo.

Alisisitiza kuwa haki za binadamu ni muhimu katika utumishi wa umma, na kwamba watumishi hao wanapaswa kuwa waadilifu.

Hata hivyo, alisema kama wilaya, wataendelea kufuata kanuni za maadili na mavazi ya ofisini ili kuhakikisha kuwa utumishi wa umma unakuwa mfano wa ufanisi, heshima, na utawala bora.

Mratibu wa mafunzo hayo, Wakili wa Serikali wa Wizara hiyo, Prosper Kisinini, alieleza umuhimu wa watendaji wa umma kuwa ni kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuepusha madhara kwa wananchi.

TULIKOTOKA,TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Kipindi cha mama na mwana kilivyotikisa RTD

Na Adam Fungamwango

WIKI mbili zilizopita tulikuwa na mada ya wanafunzi miaka ya katikati ya 1970 hadi katikati ya 1990 kukichukia mno kipindi cha 'Kumekucha' na wimbo wake ambao jina lake linafanana na kipindi.

Kisa ni kwamba tu ndiyo kipindi ambacho kilikuwa kikianza wakati wanafunzi wanatakiwa kuamka na kuwahi kwenda shule. Kutokana na mazingira na wakati uliopo walijikuta wakikichukia kipindi hicho.

Kwanza muda huo wakati wimbo huo unasikika walikuwa wanatakiwa waamke na kujiandaa kwenda shule. Halafu wakati wimbo huo unamalizika wanatakiwa wawe wameshafika shuleni na kupata namba. Vinginevyo bakora zinawahusu.

Leo tuko tofauti kidogo. Tunaangalia kipindi ambacho kilikuwa kipenzi cha wanafunzi na watoto enzi hizo. Hiki ni kipindi cha 'Mama na Mwana.'

Ni kipindi kilichpendwa mno na watoto pamoja na wanafunzi kutokana na maudhui ya kipindi chenyewe wanayofanana na umri wao pamoja na mambo ya shule.

Ni kipindi kilichokuwa maarufu sana miaka ya mwanzoni mwa 1980 hadi katikati ya miaka ya 1990.

Kilikuwa kikiendeshwa na watangazaji wa kike, ambao walikifanya kipendwe mno kutokana na jinsi wanavyotangaza, maana walijua kabisa wanaowatangazia si wakubwa wenzake, bali ni watoto ambao bado hawajaanza shule na wanaosoma.

Lugha iliyotumika ni kama ile ya mama na mtoto wake, au bibi na mjukuu wake.

Mtangazaji wa kwanza kabisa ambao hawezi kusahaulika na watoto au wanafunzi wa wakati ule ni Debora Mwenda.

Mama huyu kwa kweli alikifanya kipindi cha 'Mama na Mwana' kuwa kipindi bora ambacho hakuna mtoto aliyetaka kukikosa.

Kilikuwa kikianza Jumamosi mchana, siku ambayo watoto hawaendi shule, lakini kilirudiwa Jumapili jioni.

Muda ambao kipindi kinakaribia kuanza, watoto wanakula mapema na kukisubiri. Kikianza kila mmoja anataka kuwa karibu na redio ili asikilize nini kimeandaliwa siku hiyo.

Kwenye kipindi hicho hawakupita watangazaji wengi, nadhani Redio Tanzania Dar es Salaam, walikuwa wanataka wale tu ambao wana uwezo wa kuzungumza na hadhira ya watoto huko majumbani.

Mtangazaji mwingine ambaye naye atakumbukwa kuwa aliweza kukonga nyoyo za watoto ni Sarah Dumba.

Tukija kwenye kipindi chenyewe, pamoja na mambo ya shule kama vile masomo, kwaya, na vingine vinavyofanana na hivyo, lakini kubwa watoto walipenda mno hadithi.

Ubunifu wa RTD na Debora mwenyewe jinsi hadithi zilivyokuwa zikisimuliwa, ndiyo ulisababisha hata wakubwa nao kupenda kipindi hicho.

Hakukuwa na televisheni kipindi hicho, lakini usimuliaji wake, ulifanywa kwa namna ya maigizo hivi. Yaani kama kuna zimwi, basi ilirekodiwa sauti fulani hivi ikaongezwa na utaalam wa teknolojia ya wakati huo, basi ikaonekana sauti moja nene, nzito, yenye mikwaruzo na yenye kutisha.

Malki alikuwa na sauti yake, mfalme naye alikuwa na sauti yake, ili mradi hadithi zake zilikuwa kama tamthilia, maigizo au filamu.

Watangazaji kama Charles Hillary, Sekioni Kitojo, Michael Katembo, Nadhhir Mayoka na wengineo kwa kiasi kikubwa walitumika sana kuingiza sauti za kuigiza kwenye hadithi hizo.

Mfano Charles aliigiza kama mfanyabiashara kwenye hadithi ya 'Ua Jekundu', Mayoka aliigiza kama 'Kamal' kwenye hadithi ya 'Siri binti Mfalme'.

Ilikuwa ni burudani ya aina yake, kwani kila mmoja alikuwa akivuta taswira yake jinsi anavyoisikia hadithi. Kumbuka kuwa wakati huo kwa Tanzania Bara, televisheni ilikuwa ni ndoto ya mchana, hivyo kila mmoja alijitahidi kujiwekea televisheni yake kichwani, kuona mfanyabiashara anafananaje, na hata jitu la msituni linafananaje.

Hadithi zilizopendwa sana wakati ule ni kama hizi zilizotangulia kuzitaja 'Ua Jekundu', watoto waliita jitu la msituni, 'Siri Binti Mfalme' hadithi iliyotoka kwenye kitabu cha Alfu Lela Ulela iitwayo Kamaralzaman na Badoura binti mfalme, 'Mbalamwezi Nyota Begani', 'Jadi Mbaharia' iliyosimuliwa kutoka kwenye hadithi ya 'Sindbad Baharia', 'Binti Chura' na zingine nyingi.

Hata hivyo, hadithi ambazo kila mmoja hawezi kuzisahau kwanza kabisa ni ile ya mfanyabiashara anakwenda safari ya mbali na mabinti zake kila mmoja kuagiza zawadi, lakini wa mwisho akaagiza ua jekundu.

Baba huyo alifika kwenye jumba kubwa la ajabu lililokuwa lina kila kitu. Kwenye bustani alikutana na ua jekundu alipolichuma, lilitokea jitu kubwa lenye hasira lililotaka kumrarua, lakini mwisho ya siku lilimuachia kwa masharti ya kumruhusu binti yake mmoja kati ya watatu aje kuishi naye pale. Baba aliporudi nyumbani, binti yule yule mdogo alikubali kwenda kuishi.

Mwisho wa hadithi ilikuwa jitu lile zamani alikuwa ni Mwanamfalme aliyetupiwa uchawi na masharti yake ili apone ilikuwa ni kuliliwa machozi na binadamu.

Kumbuka binti yule alipata ruhusa kwenye kwao, akachelewa kurudi aliporejea alilikuta jitu limekufa, binti akalia sana na machozi yakamdondokea, uchawi ukaondoka na kugeuka kijana mzuri. Wakafunga ndoa.

Debora Mwenda, mtangazaji maarufu zaidi kwenye kipindi cha 'Mama na Mwana' enzi hizo, Redio Tanzania Dar es Salaam (RTD).

**Tuma meseji 0716 350534**



Debora Mwenda.

# KIVU KUSINI HOFU TUPU

## -Wanajeshi 12,000 wa Burundi wailinda




Wanajeshi wa Burundi wakiwa nchini DRC kukabiliana na waasi wa M23. **PICHA: AFP**

**Na Moshi Lusonzo**

WAKATI Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya za Afrika Mashariki na ile ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) wanakutana Dar es Salaam, kujadili mzozo wa Congo, Burundi imepeleka zaidi ya wanajeshi 10,000 Kivu Kusini.

Hata hivyo, kuna taarifa za Uganda kuwa imeongeza wanajeshi wake ndani ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) tayari kuingia katika mapambano.

Hata hivyo, serikali ya Uganda imekanusha taarifa hiyo ikisema haina ukweli wowote.

Kutoka vyanzo mbalimbali, vilieleza wanajeshi wa Burundi waliwasili katika eneo la Gatumba kwenye mpaka wake na DRC na wanatarajiwa kuwasili Mji wa Bukavu, ambao ni makao makuu ya Jimbo la Kivu Kusini.

Septemba 2023, Burundi ilitia saini makubaliano ya kijeshi na DRC, hatua ambayo imeifanya nchi hiyo kuamua kujihusisha moja kwa moja na mzozo huo unaoendelea.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo ilisema wanajeshi wa Burundi (FDNB) kati ya 10,000 hadi 12,000 tayari wameingia maeneo mbalimbali ya Kivu Kusini kupambana na waasi wa M23 wanaoungwa mkono na Rwanda.

Vyanzo vya kiusalama vilisema idadi hiyo ya wanajeshi ni kubwa na inaweza kubadili upepo wa mapambano Kivu Kusini.

Inaelezwa kwamba kuna vitengo 16 vya wanajeshi wa Burundi ndani ya DRC, kati ya hivyo vitano vipo katika miji ya Fizi na Uvira vilivyopewa majukumu ya kupambana na waasi wa RED-Tabara wenye asili ya Burundi.

Wanajeshi wengine wanatarajiwa kuweka kambi katika Mji wa Bukavu kujaribu kuwazuia waasi wa M23 kuingia kwenye eneo hilo.

**JESHI CONGO LAJIANDAA**

Duru za kivita zinaeleza wanajeshi wa jeshi la serikali linajiandaa kufanya uvamizi katika mji wa Kavumu, ambako kuna uwanja wa ndege wa mkoa wa Kivu Kusini. Baadhi ya mashirika ya kibinadamu na wakazi wa Bukavu, walisema vifaa na vikosi viliondolewa ili kuepusha kutekwa na waasi wa M23 wanaosonga mbele.

Kavumu ni kizuizi cha mwisho kabla kuufikia mji wa Bukavu, ambao uko umbali wa kiasi kilometa 30.

Mkazi mmoja ameliambia shirika la habari la Ufaransa (AFP), alisema hofu imetanda kwa watu wanaoishi katika miji inayopakana na uwanja huo wa ndege.

M23 wahutubia Goma

Kundi la waasi la M23, limefanya mkutano wa hadhara mjini Goma jana, huku kiongozi wao Corneille Nangaa, akisisitiza watasonga mbele hadi Kinshasa.

Shughuli za kawaida katika mji huo zilitatizwa kwa saa kadhaa, wakati waasi hao walipokuwa wakihutubia umati wa watu waliokusanyika katika uwanja wa michezo.

Akiwa mbele ya wananchi waliohudhuria mkutano huo, Nangaa, alitambulisha safu mpya ya uongozi wa mkoa huo akiwamo Bahati Musanga Erasto kuwa Gavana, akisaidiwa na Wily Manzi na Amani Bahati.

Aidha, alisisitiza uongozi wa M 23 utaimarisha uhusiano wa karibu na wananchi kwa lengo la kutatua changamoto zinazowakabili.

**RAMAPHOSA ATOA KAULI**

Akizungumza kuhusu uwepo wa wanajeshi wa Afrika Kusini nchini DRC, Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, alisema suluhu ikipatikana wanajeshi hao watarudi nyumbani.

Katika hotuba yake kwa taifa hilo juzi usiku, Rais Ramaphosa, ambaye anakabiliwa na shinikizo la kutakiwa kurudisha jeshi nyumbani baada ya wanajeshi 14 kuawa na M23, alisema ni lazima suluhu ya amani ipatikane.

Afrika Kusini imetuma zaidi ya wanajeshi 1,000 katika kikosi cha Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kusaidia jeshi la DRC kupambana na waasi wa M23.

"Tunatoa wito kwa pande zote kuafiki juhudi za kidiplomasia zinazoendelea za kutafuta suluhu ya amani, ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa mazungumzo ya Luanda." Alisema.

Hata hivyo, alithibitisha kuwa atahudhuria mkutano wa wakuu wa EAC na SADC unaofanyika leo jijini Dar es Salaam.

"Tutasisitiza wito wetu wa kusitishwa kwa uhasama na kuanza tena mazungumzo ili kufikia suluhu ya kweli na ya kudumu, tutajitahidi kuhakikisha wanajeshi wetu wanarejea nyumbani."

Baadhi ya wabunge wa Bunge la Afrika Kusini wiki hii walilaani uamuzi wa nchi hiyo kupeleka wanajeshi wake DRC.

Wizara ya Ulinzi bado haijapata miili ya wanajeshi waliouawa.

Afrika Kusini, Malawi na Tanzania ni nchi za SADC ambazo zina wanajeshi wanaosaidia serikali ya Congo.

Tayari Rais wa Malawi alitangaza kuondoa jeshi la nchi yake kutoka DRC.

**UN YATOA ONYO**

Umoja wa Mataifa umetoa wito kuwapo kwa amani licha ya waasi wa M23 wanazidi kusonga mbele.

Waasi hao wanaoungwa mkono na Rwanda jana waliendelea kusonga mbele katika eneo la mashariki mwa Congo na walionekana wakijiandaa kuuteka mji muhimu wa kimkakati.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, alihimiza kusitishwa kwa mapigano haraka ili kuepusha maafa kwa raia kama ilivyokuwa mji wa Goma hivi karibuni.

Akizungumza katika makao makuu ya Umoja wa Mataifa mjini New York, Guterres alisema ni wakati wa kuufikisha mwisho mgogoro huo.

Alisisitiza kuna umuhimu wa kufikia makubaliano ya pamoja kwa ajili ya amani.

**MAWAZIRI WAKUTANA**

Mawaziri wa SADC na Jumuiya ya Afrika Mashariki EAC jana walikutana jijini Dar es Salaam, kujadili mzozo wa Congo, kabla ya leo viongozi wakuu wa jumuiya hizo kufanya mazungumzo.

Kongamano hilo linatarajiwa kutafuta suluhu ya mzozo unaoendelea mashariki mwa DRC.

Waasi wa M23 wanaoungwa mkono na Rwanda, ambao wameuteka mji wa mashariki wa Goma, wanaendelea kukabiliana vikali na majeshi ya serikali.

Kulingana na Umoja wa Mataifa zaidi ya miili 2,000, imekutwa ikizagaa katika mitaa ya mji wa Goma, baada ya M23 kuteka na kuudhibiti.

# MATUKIO KATIKA PICHA



Ofisa Uchaguzi Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Zaituni Said (wa tatu kulia), akizungumza katika ufunguzi wa semina ya mafunzo ya uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura wilayani humo juzi, baada ya maofisa uandikishaji wasaidizi ngazi ya jimbo na kata kula kiapo. Wengine ni Ofisa Mwandikishaji Msaidizi ngazi ya Jimbo, Ruth Mwelo (kulia), Ofisa Mwandikishaji wilaya, Dk. Jumaa Mhina na wa pili kushoto ni Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya wilaya hiyo, Lusajo Mutua. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akitia saini kitabu cha maombolezo ya msiba wa marehemu Sekunda Massawe ambaye ni mama mzazi wa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alipowasili msibani katika kijiji cha Nduweni Tarakea, wilayani Rombo, mkoani Kilimanjaro, juzi. **PICHA: OMR**



Katibu wa Idara ya Mambo ya Nje na Waziri Kivuli wa Viwanda na Biashara wa Chama cha ACT-Wazalendo, Wakili Mwanaisha Mdeme, akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam juzi, kuhusu nia yake ya kugombea ubunge Jimbo la Kigamboni katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu. **PICHA: IMANI NATHANIEL**



Rais wa Zanzibar, Alhajj Dk. Hussein Ali Mwinyi, akijumuika na viongozi wa Jamaat la Shia Ismailia Zanzibar katika kuitikia dua ikisomwa na Mukhi Murad Vellani, baada ya kutia saini kitabu cha maombolezi kufuatia kifo cha Kiongozi Mkuu wa 49 wa Madhehebu ya Shia Ismailia Duniani na Mwanzilishi wa Mtandao wa Maendeleo wa Aga Khan (AKDN), Prince Karim Al -Hussaini Aga Khan IV, aliyefariki dunia Jumanne wiki hii, jijini Lisbon Ureno, alipofika katika Jamaat la Shia Ismailia Zanzibar Hurumzi, Wilaya ya Mjini Unguja jana. **PICHA: IKULU**



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Ridhiwani Kikwete (katikati), akijadiliana na Mbunge wa Jimbo la Ushetu, Emmanuel Cherehani (kulia) na Mbunge wa Viti Maalumu CCM, Janejery James, katika viwanja vya Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# HADITHI

# Malaika shetani-7

WAKATI mwingine umdhaniavyo binadamu sivyo alivyo. Unaweza kumuona ni mtu mbaya au ana roho mbaya kwa kumuangalia, lakini akawa ni mtu mzuri sana ambavyo hukupata kudhani. Unawezi kukutana na mtu ambaye kwa muonekano na jinsi anavyokutendea ukamuona ni mtu mwema sana. Hata hivyo ndani ya roho yake ana mambo ambayo akikifungulia unaweza kuanguka na kuzirai. Ni mtu mbaya kuliko ubaya wenyewe. Anaficha ukatili na roho yake mbaya kwa kivuli cha kujifanya mwema. Watu hawa ni hatari sana. Kwenye kijiji kimoja kilichopo Bungu, Rufiji kunatokea mauaji ambayo hayajulikani chanzo ni nini. Mauaji hayo yanawahusisha wasichana wawili wanaosoma shule ya sekondari, pamoja na vijana kadhaa. Wananchi wanataka serikali ya kijiji ichukue hatua kwa kuwasaka wauaji ambao wanakitia hofu kijiji cha Mikamba na vya jirani. Je muuaji atapatikana? Ni nani? Fuatilia mkasa huu.

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

Zuhura aligoma. "Nitakwenda mwenyewe, rudi nyumbani kwa usalama wako." Zuhura sasa alianza kuwa mwalimu wa Feruzi, wakati mwanzo alimwona kama mlaghai. "Hapana. Wewe ni mpenzi wangu, kama wataniua mbele yako sawa." Alimjibu huku akimshika mkono na kuanza kumsindikiza kwao. Walipofika hatua kadhaa kabla ya kufika nyumbani, waliagana na kukumbatiana na mabusu moto moto, "Mungu akulinde mpenzi wangu huko uendako. Akitangulie na mabaya yote, urejee mapema tuoane. Enhee kwanza nimesahau." "Umesahau nini Zuhura tena?" "Utarudi wakati gani? Na utajuaje kama huku mambo yamepoa? Na wanaokutafuta unadhani hata ukikaa miaka mitatu ukirudi ndiyo wataacha kukumaliza kama watakuwepo?" "Da! Umeuliza swali zuri kweli mpenzi wangu. Sikutegemea swali kama hili. Ni kwamba mimi nakwenda huko. Lakini nikifika nitatafuta mtu yoyote au mwanausalama, polisi ambaye atakuwa tayari kunisikiliza kwa hili linalolisema ili aje kulimaliza huku. Kuwakamata wote waliohusika. Hapo ndipo nitakaporudi." "Unadhani ni rahisi kiasi hicho?" "Si rahisi, lakini ninajitahidi." "Basi sana, nitafurahi kwa sababu mimi Naima alikuwa shoga yangu mkubwa, nimehuzunika sana na kifo chake." Waliagana. Ilikuwa ngumu kidogo kuachana, lakini ilikuwa lazima waachane. Feruzi alisubiri hadi Zuhura alipofunga mlango. Haikuwa rahisi, kwani Zuhura alichelewa kuufunga kutokana na kutaka tu kumuona Feruzi angalau kwa mara ya mwisho, kwani alitarajia kuwa atamuona tena baada ya muda mrefu kupita, au asimuone tena.

Wakati anarejea, Feruzi alihisi kama kuna watu wanamfuata kwa nyuma.

Haraka akatoka kando ya njia, na kujitoma kwenye majani. Akaona haitoshi, akapiga hatua kadhaa na kujiingiza kwenye rundo la majani yaliyojikusanya pamoja. Ni muda huo huo, macho yake mawili yalishuhudia watu wawili warefu, mmoja akiwa na panga na mwingine mkuki. "Alikuwa hapa hapa." Mmoja alisema akimwambia mwenzake. "Hata mimi nimemwona. Sasa ametoweka vipi kama mzimu?" Aliyejibu akauliza. "Nadhani hajaenda mbali. Yupo hapa hapa, tumsubiri." Jibu hilo lilikuwa kama msumari kwenye kidonda cha Feruzi. Aliona kama wakikaa eneo lile hawezi kutoka hapo hadi kutakapopambazuka




**"Shoga yangu, kumbe kile kifo cha Naima kilikuwa na mkono wa mtu. Kuna mkubwa mmoja anahusika. Ametuma vijana kwa kuwalipa pesa ili wamuue. Mpenzi wangu Feruzi aliwafuma wakiwa wanataka kumfukia baada ya kumuua. Wakaiacha maiti na kumkimbiza yeye. Hawakurudi tena eneo lile kwa kuhofia kukamatwa. Ndiyo maana maiti ya Naima ilipatikana, lakini ilikuwa ifukiwe ili kuua ushahidi.**

na kukishakuwa kweupe, watamuona. Pamoja na hayo aliamua kujibanza pale pale, akikumbana na shuluba za mbu wanene, walishiba ambao walianza kunyonya damu yake ya moto. Hakuthubutu kujipiga mwilini ili kuwaondoa. Kitendo chochote cha kufanya hivyo, ni kuwapa ishara maadui zake kuwa windo lao lipo eneo hilo. Nusu saa baadaye aliwaona wakiondoka taratibu kuelekea kule alikotoka. Walitokomea na macho yake hayakuwashuhudia tena. Aliendelea kukaa kwenye kichaka kwa dakika 10 zingine. Hakujidanganya kuwa watakuwa wameondoka moja kwa moja. Alijua utakuwa ni mtego tu. Baada ya kuona kimya kinaendelea, alijichomoa kutoka kichakani. Hakuthubutu kutaka kupita njiani. Kitendo chochote cha kufuata njia, ilikuwa ni kukifuata kifo chake mwenyewe. Alianza kutokomea kwenye majani. Alipita kichaka kwa kichaka. Pamoja na kwamba ni usiku, mkusanyiko wa moto, vichaka na majani vilijengwa taswira ya kutisha, vikihanikizwa na sauti za wadudu na ndege mbalimbali waliokuwa wakilia usiku. Kwake ilikuwa afadhali zaidi kuliko kukutana na wale watu waliokuwa wanamsaka. Ilionekana walikuwa wakimsaka na walimwona, huenda hakiwa peke yake, au na mpenzi wake Zuhura. Alianza kuwa na wasiwasi na usalama wa mpenzi wake. Huenda wale watu wanaweza kwenda kwake na kumlazimisha aseme alikokwenda. Hata hivyo hakuthubutu kutaka kurejea. Alionekana kuwa yupo karibu na hatari zaidi ya kuuawa. Mara moja ameponyeka. Hii ni mara ya pili ambayo nayo bado haijaisha. Hana uhakika kama anaweza kuliona jua ya kesho asubuhi. Ikampa nguvu ya kuzidi kutokomea.

*******************************

Kijiji cha Bungu kiliamka na taarifa zingine mbaya za msiba. Ni wiki moja baada ya kifo cha Naima, kikatokea kifo cha msichana mwingine, Zuhura. Aliokotwa kando ya kisima cha kijiji, akiwa amenyongwa. Na katika hali ya kushangaza, kijana mmoja anayesadikika kuwa ndiye alikuwa mpenzi wake, Feruzi, ametoroka kijijini hapo. Hilo lilifanya wanakijiji wote wajue kuwa, Feruzi ndiye aliyemnyonga mpenzi wake na kukimbia.

Msiba huo ulikumbushia msiba mwingine uliotokea siku chache zilizopita wa msichana mrembo, Naima.

Watu walijazana kwenye msiba na taratibu zote za mazishi zikafanyika, Zuhura, akazikwa kwa heshima zote.

Kwenye salamu za pole na rambirambi, uongozi wa kijiji ulisema kuwa tayari viashiria kwa nani anahisika kwenye mauaji ya wasichana hao yameanza kuonekana.

"Kuna kijana anaitwa Feruzi, ametoweka. Huyu kijana hapa anajulikana kuwa na mahusiano ya kimapenzi na Zuhura. Haiwezekani, Zuhura ananyongwa, halafu mpenzi wake haonekani, na kuna taarifa majuzi walikuwa wote," alisema msemaji wa uongozi wa kijiji.

"Hapa sasa tunaanza kupata wasiwasi hata wa mauaji ya Naima, huenda huyu kijana na kundi lake wanahusika," alisema msemaji huyo mbele ya halaiki ya wanakijiji hicho na jirani zao.

Kilichotokea ni kwamba, siku moja baada ya Feruzi kuondoka, Zuhura alikuwa katika hali mbaya na ya wasiwasi. Hakuweza kuweka kitu moyoni. Alimfuata shoga yake Tefa na kumwambia kila kitu kilichotokea.

"Shoga yangu, kumbe kile kifo cha Naima kilikuwa na mkono wa mtu. Kuna mkubwa mmoja anahusika. Ametuma vijana kwa kuwalipa pesa ili wamuue. Mpenzi wangu Feruzi aliwafuma wakiwa wanataka kumfukia baada ya kumuua. Wakaiacha maiti na kumkimbiza yeye. Hawakurudi tena eneo lile kwa kuhofia kukamatwa. Ndiyo maana maiti ya Naima ilipatikana, lakini ilikuwa ifukiwe ili kuua ushahidi. Walianza kufuatilia ni nani, baadaye wakafahamu kuwa ni Feruzi, wakaanza kumwinda ili wamuue asije kutoa siri ya wale vijana waliowaona kwa sababu anawafahamu kwa wote kwa sura na wengine wanaishi hapa, wengine vijiji vya jirani. Mpenzi wangu kaona isiwe shida, kaamua kukimbia kifo. Hivi navyokwambia shoga yangu hayupo kijiji hiki. Kijiji kimechafuka."

Maneno haya yaliwafikia wenyewe. Wakajua kuwa aliyekuwa akisambaza ni Zuhura. Wakamuua. Lengo ni kuzuia taarifa kusambaa na kuwatia hofu wote ambao wana nia ya kufuatilia au kusambaza taarifa hizo. Na kweli kila mmoja sasa kijijini Bungu, akaendelea na hamsini zake. Kufuatilia tena habari za kifo cha Naima, hata cha Zuhura, ni sawa na kufuatilia kifo chako mwenyewe.

**Itaendelea Jumamosi**

# ALIYEMTUNGUA DIARRA ANAAMINI KENGOLD FC HAITASHUKA DARAJA

**Na Somoe Ng'itu**

LICHA ya kuendelea kuburuza mkia katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, nyota wa KenGold FC ya jijini Mbeya, Selemani Bwenzi, amesema anaamini timu yao itabakia katika ligi hiyo kwa msimu mwingine tena.

Bwenzi alifunga bao la kufutia machozi la KenGold katika mechi iliyomalizika kwa kupokea kichapo cha mabao 6-1 kutoka kwa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga.

Nyota huyo alipiga mpira wa moja kwa moja kutoka katikati ya uwanja ambapo KenGold ilikuwa inaanzisha mchezo baada ya kufungwa bao la sita na mpira huo ukatinga wavuni moja kwa moja kufuatia kipa, Djigui Diarra, kushindwa kuudaka.

Akizungumza na gazeti hili jana, Bwenzi alisema mechi zilizobakia katika msimu huu ni nyingi na lolote linaweza kutokea na hivyo timu yao ikasalimika na janga la kushuka daraja.

**Bwenzi alisema hakuna mechi nyepesi, hivyo katika kila mchezo wanaocheza wamejiandaa kupambana kusaka matokeo chanya na anaamini watafikia malengo.**

"Ligi bado changa, kuna mechi nyingi zimebakia huko mbele kabla ya kumaliza msimu, tutaendelea kupambana na kujifunza ili kupata matokeo mazuri, wachezaji na benchi la ufundi kila mmoja anajua nini tufanye ili tusishuke daraja," alisema mchezaji huyo.

Aliongeza matokeo mabaya waliyopata dhidi ya Yanga yamechangiwa na kuingia uwanjani bila kuwaheshimu wapinzani wao.

"Tuliingia uwanjani bila kuwaheshimu Yanga, wakatuadhibu," aliongeza mchezaji huyo.

Alisema wanarejea katika uwanja wa mazoezi ili kurekebisha upungufu uliopo na kurejea katika mechi ijayo wakiwa imara.

KenGold inarejea jijini Mbeya kwa ajili ya kujiandaa kuwakaribisha Fountain Gate kutoka Dodoma katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Jumatatu kwenye Uwanja wa Sokoine.



Kocha wa timu ya vijana (jina lake halikupatikana) akitoa maelekezo kwa wachezaji chipukizi wanaolelewa katika Kituo cha Michezo cha JMK Park kilichoko jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA : JUMANNE JUMA**

# JKU yazinduka Ligi Kuu Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya JKU SC imeendelea kujiimarisha baada ya kuichapa Inter Zanzibar mabao 3-0 katika mechi ya Ligi Kuu ya Zanzibar iliyochezwa kwenye Uwanja wa Cairo ulioko Kiwengwa, juzi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa JKU, Mselem Sultani, alisema matarajio yao makubwa katika mzunguko huu ni kufanya vizuri baada ya kushindwa kufanya hivyo katika mechi za mapema msimu huu.

Sultani alisema kila mechi wanayocheza katika mzunguko huu wanaichukulia 'uzito mkubwa' bila kuangalia mpinzani wanayekutana naye yuko katika nafasi gani kwenye msimamo wa ligi hiyo.

"Tulijiandaa vizuri sana kuikabili Inter Zanzibar, niliwaeleza wachezaji wangu wanatakiwa kucheza kwa umakini mkubwa ili kutopoteza lengo la kupata ushindi, tunashukuru tulifanikiwa," Sultani alisema.

Kocha huyo aliongeza wanafahamu wanapokutana na timu zilizo katika hatari ya kushuka daraja mechi huwa ngumu zaidi kinachotakiwa kufanyika ni kuwabadilishia mbinu.

"Bado tunahitaji kushinda zaidi ili kupanda juu katika msimamo wa ligi, ingawa hatukuwa na mwanzo mzuri lakini tunataka tuwe na mwisho mzuri wakati msimu wa ligi utakapomalizika," kocha huyo alisema.

Aliongeza kwa sasa anarudi katika uwanja wa mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mzunguko wa 18 wa ligi hiyo ambayo watashuka dimbani Februari 14, mwaka huu kucheza dhidi ya Zimamoto.

# 'Waishukuru Simba SC ikiwafunga Namungo'

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Tabora United, Anicet Makiadi, amesema mechi waliocheza dhidi ya Simba imewasaidia kupata ushindi wa mabao 2-1 katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Namungo FC uliochezwa Jumatano iliyopita kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani Tabora.

Jumapili iliyopita, Tabora Sugar ikiwa nyumbani ilifungwa mabao 3-0 na Simba.

Makiadi aliliambia gazeti hili jana, licha ya kupoteza mechi dhidi ya Simba, lakini iliwapa nafasi ya kujifunza vitu vingine ambavyo wamevitumia na kusaidia kupata pointi tatu hapo juzi.

"Niliwaahidi mashabiki wa Tabora kuwa baada ya mechi dhidi ya Simba, tutashinda mechi inayofuata na kweli tumefanya hivyo, furaha imerudi baada ya wiki iliyopita kuhuzunika, kikubwa mchezo wetu ule ulitufunza vitu vingi, unapocheza na timu kubwa kama ile kuna mengi ya kujifunza na kuangalia udhaifu wako.

Ni timu ambayo inaweza kukufanya kocha kubaini matatizo ya timu yako yalipo na kweli tuliona tutayatatua mazoezini, pia hata wao unawaangalia jinsi gani wanavyocheza, unatumia staili yao kucheza na timu nyingine inaweza kukupa matokeo, na tumefanya hivyo," alisema kocha huyo raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DR Congo).

Mfungaji wa moja ya mabao katika mchezo huo, Mkongomani, Heritier Makambo, alisema haikuwa mechi rahisi kwani Namungo imeonekana kuimarika kwenye mzunguko wa pili, hasa baada ya kufanya usajili kipindi cha dirisha dogo.

Alisema ilibidi wabadilishe mfumo wa uchezaji kwa kupitia pembeni badala ya katikati, ndipo walipofanikiwa.

"Tumecheza na Namungo ambao inaonekana wametengeneza timu nzuri, tuliruhusu bao la kwanza, lakini hatukukata tamaa, tuliendelea na mchezo tukapata mabao mawili.

Mabao yetu yote mawili yalitokea pembeni kwa sababu wapinzani wetu walionekana kutuzuia sana katikati mwa uwanja, tukaona sasa tutumie mipira ya faulo au tupitie pamebeni kwa sababu tuna wachezaji wazuri wa kupiga vichwa na wapiga krosi wazuri," alisema.

Nahodha wa Namungo, Erasto Nyoni, alisema wamepoteza mchezo huo kutokana na kutokuwa makini, hasa baada ya kutangulia kupata bao.

"Mchezo ulikuwa mgumu, tulifanikiwa kupata bao la mapema, lakini baadaye tulikosa umakini wenzetu kurudisha na kufunga bao la pili, ila tutajirekebisha," alisema.

Jacob Massawe, alianza kuifungia Namungo bao la kwanza, kabla ya Offen Chikola kusawazisha dakika ya 32 na Makambo kutupia la pili, dakika ya 52.

Matokeo hayo yanaifanya Tabora United kuendelea kujichimbia nafasi ya tano, ikifikisha pointi 28, huku Namungo ikibaki na pointi zake 17, ikiwa nafasi ya 12.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### GUEHI ANUKIA CHELSEA

CHELSEA ina imani beki wa Crystal Palace na England, Marc Guehi, mwenye umri wa miaka 24, atajiunga nao badala ya kuelekea Tottenham Spurs msimu wa joto. (*TBR Football*)

### DAU LA ISAK LATAJWA

KLABU ya Newcastle United inakadiria thamani ya mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Sweden, Alexander Isak, mwenye umri wa miaka 25 ni pauni milioni 150. (*Fichajes*)

### CHELSEA KUMUUZA SANTOS

CHELSEA iko tayari kumuuza kiungo wa Brazil, Andrey Santos, mwenye umri wa miaka 20, ambaye yuko Strasbourg kwa mkopo, mwishoni mwa msimu huu. (*Team Talk*)

### ARSENAL YAWAKACHA WAPYA

ARSENAL iliwafuatilia wachezaji wanne wakati wa usajili wa dirisha la Januari, lakini ikaamua kutomsajili mchezaji yeyote kwa sababu hawakupata chaguo bora. (*Mail*)

### NEWCASTLE: TRIPPER HAUZWI

NEWCASTLE United imekataa ombi la Galatasaray kuhusu uhamisho wa beki wa England, Kieran Trippier mwenye umri wa miaka 34. (*Caughtoffside*)

### MATETA AIVUTIA UNITED

MANCHESTER United, Chelsea na Newcastle United zinavutiwa na mshambuliaji wa Crystal Palace na Ufaransa, Jean-Philippe Mateta, mwenye umri wa miaka 27, ambaye bado hajasaini mkataba mpya. (*TBR Football*)

### DEWSBURY-HALL BEI CHINI

CHELSEA inatarajiwa kupunguza bei kwa kiungo wa kati wa England, Kiernan Dewsbury-Hall, mwenye umri wa miaka 26, baada ya mazungumzo ya uhamisho kushindikana Januari. (*Football Insider*)

### UNITED YAMTAKA DELAP

KLABU ya Manchester United imejitosa kwenye kinyang'anyiro cha kumsajili mshambuliaji wa Ipswich na England, Liam Delap, mwenye umri wa miaka 21, ambaye pia amekuwa akihusishwa na Tottenham Hotspur. (*Express*)

### HENDERSON ALIKATALIWA

AJAX ilikataa kumruhusu kiungo, Jordan Henderson, mwenye umri wa miaka 34, kuhamia Monaco kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili. (*Mail*)

### GLASNER ATAKIWA PALACE

KOCHA wa Crystal Palace, Oliver Glasner, anataka kumsajili kiungo wa AC Milan na Serbia, Strahinja Pavlovic, mwenye umri wa miaka 23, kwa mkataba wa pauni milioni 25. (*Sun*)

### TZIMAS KUTUA BRIGHTON

KLABU ya Brighton inakaribia kumsajili mshambuliaji wa PAOK na Timu ya Taifa ya Ugiriki, Stefanos Tzimas, mwenye umri wa miaka 19, ambaye yupo Nurnberg kwa mkopo . (*Sky Sports*)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# AMORIM AANIKA SIRI RASHFORD KUONDOKA

**MANCHESTER,** England

**Ni kwa sababu mshambuliaji huyo alishindwa kubadilika ili...**

RUBEN Amorim amesema mshambuliaji, Marcus Rashford, alilazimika kuondoka Manchester United kwa sababu hakuweza kufuata mawazo yake.

**Rashford alijiunga na Aston Villa kwa mkopo hadi mwisho wa msimu baada ya kukosa nafasi katika kikosi cha Amorim.**

Na kocha huyo wa United amedokeza kwa sababu mchezaji huyo wa kimataifa wa England mwenye umri wa miaka 27, hakumudu kasi yake, ilibidi aondoke klabuni hapo.

"Ninachosema sikuweza kumweka Marcus kuona jinsi anavyotakiwa kucheza soka na kujifua, jinsi ninavyoiona," alisema Amorim.

"Na wakati mwingine una mchezaji mmoja ambaye ni mzuri sana na kocha mmoja na mchezaji sawa na kocha mwingine ni tofauti. Nawatakia kila la heri Rashford na Unai Emery, na wanaweza kuungana kwa sababu ni mchezaji mzuri sana."

Rashford alifunga bao la kwanza chini ya utawala wa Amorim katika sare ya 1-1 Uwanja wa Ipswich Town Novemba, mwaka jana. Pia alianza katika mechi dhidi ya Everton na Viktoria Plzen.

Lakini baada ya kuondolewa kwenye kikosi cha dabi ya Manchester hapo Desemba, mwaka jana, alijumuishwa katika kikosi kimoja zaidi cha siku ya mechi kabla ya kuruhusiwa kuhamia Villa Park.

"Kisa baadhi ya watu hawabadiliki jinsi ninavyoona soka, watu wengine wanabadilika na tunajaribu kujenga timu," alisema Amorim.

"Ni kitu ambacho unahisi, kama kocha na mchezaji. Ni kawaida kabisa, ilitokea na makocha wengi. Jambo la muhimu niko hapa nikisema ulikuwa uamuzi wangu."

# Flick amwaga sifa kwa Torres




**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa Barcelona, Hansi Flick, alisifu uwezo wa Ferran Torres wa kujaza nafasi ya Robert Lewandowski baada ya fowadi huyo kufunga 'hat trick' katika ushindi wa mabao 5-0 katika mechi ya robo fainali ya Copa del Rey dhidi ya Valencia iliyochezwa kwenye Uwanja wa Mestalla, juzi.

Fermín López na Lamine Yamal pia walifunga wakati Barca ikijiunga na Real Madrid, Atlético Madrid na Real Sociedad katika droo ya nusu fainali itakayofanyika Jumatano.

Mabao matatu ya Torres yalifikisha idadi yake ya msimu hadi 11 katika mashindano yote, huku Flick akizidi kumtumia winga huyo kama mshambuliaji wa kati akimpumzisha Lewandowski.

"Ni muhimu kila mtu aonyeshe ubora wake," alisema Flick katika mkutano na waandishi wa habari alipoulizwa kuhusu Barca kutopoteza wakati Lewandowski hayupo uwanjani.

"Ferran, uchezaji wake ulikuwa mzuri sana. Kama namba tisa, ninahesabu alifunga mabao na amefanya vizuri sana leo (juzi).

"Nina furaha kwa sababu alifunga mabao matatu. Inashangaza kwa sababu hakuwa na wakati rahisi msimu huu. Alirejea baada ya kuumia na nina furaha kwake, alikuwa mzuri leo (juzi)."

Torres alikuwa mmoja wa wachezaji kadhaa waliokuja kwenye kikosi cha Barca huku Flick akibadilisha kikosi chake, ambapo López, Frenkie de Jong na Eric García pia wakianza.

Mabadiliko hayo hayakuathiri mdundo wa Barca walipofuata kuifunga Valencia mabao 7-1 kwenye LaLiga wiki mbili zilizopita kwa kuwa mbele kwa mabao 4-0 Mestalla ndani ya dakika 30 za kwanza.

"Sasa ni muhimu kuonyesha kina hicho kwa sababu tuna wiki na miezi migumu hadi mwisho wa msimu," alisema kocha huyo wa Ujerumani.

"Nina furaha kama mechi dhidi ya Valencia nyumbani katika LaLiga. Leo (juzi) tulianza tangu mwanzo tukiwa makini sana, tukatengeneza nafasi nzuri na kufunga mabao."

# De Jong atakiwa Saudia

**BARCELONA,** Hispania

KIUNGO wa kati wa Barcelona, Frenkie de Jong amethibitishwa kufanya mazungumzo ya "mara kwa mara" kuhusu kutakiwa na klabu ya Al Ittihad inayoshiriki Ligi Kuu ya Saudia Arabia.

Uchezaji wa De Jong pale Barcelona haujawa kwenye kiwango kikubwa baada ya kupona jeraha baya la kifundo cha mguu ambalo alilipata msimu uliopita, na kumfanya akose michuano ya Euro 2024.

Mholanzi huyo ameanza mara mbili pekee kwenye LaLiga msimu huu, ingawa ameiongoza timu kama nahodha mara zote mbili.

Mkataba wake utaendelea hadi mwaka 2026 na Barcelona wanaripotiwa kutishia kumuuza mchezaji yeyote ambaye anafikia mwaka wa mwisho wa mkataba wake bila kukubaliana kuongezwa tena.

De Jong aliyejiunga na Barca mwaka 2019 kutoka Ajax anachukuliwa kuwa mali inayoweza kuuzwa wakati wa shida mbaya zaidi za kifedha za Barcelona, mara kwa mara amekataa kuihama klabu hiyo.

Barcelona ilifikia makubaliano ya uhamisho na Manchester United katika msimu wa joto wa 2022, kabla ya mazungumzo kuvunjika.

Hali ya sintofahamu inayoendelea juu ya hatima ya mchezaji huyo imechochea uvumi kuhusu kitakachofuata, huku Ligi Kuu ya Saudia ikionekana kumwania kiungo huyo.

"Mazungumzo haya ya kujua jinsi soko linavyofanyika yamekuwa ya mara kwa mara," alisema Ramon Planes, Mkurugenzi wa Soka wa Al Ittihad na Mtendaji wa zamani wa Barcelona, akiiambia Esports COPE alipoulizwa kuhusu De Jong.

"Ana furaha sana akiwa Barcelona, amezoea na si rahisi kwa mchezaji ikiwa mambo yanakwenda vizuri kuondoka kwenye timu bora kama Barca. Siku zote lazima niulize kuhusu wachezaji na uwezekano wa soko."



# Van Dijk: Tumeshinda, ila hatukucheza vizuri


**LIVERPOOL,** England

LIVERPOL iliishinda Tottenham Hotspur mabao 4-0 na kutinga fainali ya Kombe la Carabao, lakini nahodha, Virgil van Dijk alisema alisikitishwa na uchezaji wa timu yake wakati wa ushindi huo mkubwa.

Mabao ya Cody Gakpo, Mohamed Salah, Dominik Szoboszlai na Van Dijk yaliiwezesha Liverpool kuisambaratisha timu ya Kocha Ange Postecoglou, kwenye Uwanja wa Anfield.

Liverpool walionekana kucheza kwa kasi tangu dakika ya kwanza na Spurs walishindwa kupiga shuti lililolenga lango kwenye mechi hiyo, lakini Van Dijk alikosoa mchezo wao wa kipindi cha kwanza.

"Tulihitaji uchezaji kamili. Bado nadhani wakati wa mapumziko tungeweza kupata kiwango cha juu kulingana na kiwango na kuwaweka chini ya shinikizo zaidi na ndivyo nilivyosema," alisema Van Dijk akiiambia Sky Sports.



"Lakini kushinda hapa kama tulivyofanya usiku wa leo (juzi) ni jambo zuri kwa timu na klabu na sasa tunaangalia Kombe la FA." Van Dijk aliongeza: "Tulitaka kuanza kwa nguvu nyingi na nadhani mchezo ulikatizwa mara kadhaa katika kipindi cha kwanza. Inaharibu kasi kidogo iliyokuwa pale.

Matokeo hayo yanaweka hai nafasi ya Liverpool kushinda mataji yote manne makubwa msimu huu, huku ikiongoza msimamo wa Ligi Kuu England kwa pointi sita.

Pia inatarajiwa kufuzu kwa hatua ya 16 bora katika Ligi ya Mabingwa Ulaya na kukutana dhidi ya timu ya Championship, Plymouth Argyle katika raundi ya nne ya Kombe la FA hapo kesho.

Slot alisema alifurahishwa sana na juhudi za wachezaji wake kwa kile walichoonyesha kwenye mchezo dhidi ya Spurs.

Liverpool itacheza na Newcastle katika fainali ya Kombe la Carabao Machi 16, mwaka huu.

HABARI MICHEZO

## Yanga, Coastal Union kukutana Kombe FA

INATOKA UKURASA 24

"Duniani kote hakuna straika ambaye hakosi mabao, hata Ronaldo, Messi, Haaland, ziko mechi hata wanakosa, lakini kwa Dube stori kubwa kwake inakuwa ni kukosea kuliko kupatia, amefunga mabao mawili na kutoa 'asisti' moja, lakini bado anahukumiwa kwa kukosa," alisema Kamwe.

Alisema huenda suala hili linafanyika kimkakati ili kumwondoa mchezoni na kumfanya asiwe anajiamini anapokuwa uwanjani.

"Inawezekana hili inafanyika kimkakati na watu wasiotutakiwa mema ili kumfanya apunguze kujiamini, ninawaomba wanachama na mashabiki wa Yanga, hizi ndiyo nyakati za kuungana wote, na kushirikiana na wachezaji wetu ili watupatie matokeo mazuri," Kamwe alisema.

Moja ya nafasi ya wazi aliyokosa na kujadiliwa zaidi ni ile akiwa yeye na kipa wa KenGold, baada ya kuwekewa pasi ya upendo na Clatous Chama, katika mchezo uliopigwa Jumatano iliyopita, Yanga akipata ushindi wa mabao 6-1.

Katika hatua nyingine, Kamwe alisema kocha mpya wa timu hiyo, Miloud Hamdi, ameanza kazi na kikosi hicho kuelekea katika mchezo wa Ligi Kuu Bara dhidi ya JKT Tanzania utakaochezwa keshokutwa.

Alisema kocha huyo tayari ameshaanza programu yake ya mazoezi baada ya kumalizika kwa mchezo dhidi ya KenGold.

"Tunakwenda kucheza mchezo wetu mwingine dhidi ya JKT Tanzania kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, maandalizi yanakwenda vizuri, kocha wetu mpya alianza programu ya mazoezi baada ya mechi dhidi ya KenGold, tunaamini kipindi hiki alichoanza, akishirikiana na Abduhamid Moalin na wasaidizi wengine aliowakuta, tutakuwa na maandalizi mazuri," alionge-za.

Alisema wanajua mechi hiyo haitakuwa rahisi kwa sababu wanakwenda kucheza na timu nzuri, yenye wachezaji wazoefu na Ligi Kuu na timu ngumu inapocheza nyumbani kwao.

"Msimu uliopita tulipata suluhu nyumbani kwao, tuna hiyo rekodi kwa hiyo safari nii tunakwenda kwa tahadhari zaidi na nguvu kubwa ili tupate ushindi," Kamwe aliongeza.

Yanga ndio wa ligi hiyo wakiwa na pointi 45 kibindoni huku watani zao, Simba yenye pointi 44 wakifuatia, kila timu imecheza michezo 17.

# TAOUSSI ACHEKELEA USHINDI, UBORA WA NYOTA AZAM FC

**Na Somoe Ng'itu**

BAADA ya timu yake kupata ushindi wa mabao 2-0 katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC hapo juzi, Kocha Mkuu wa Azam FC, Rachid Taoussi, amefurahishwa na namna wachezaji wake walivyojituma na kucheza kwa bidii katika mchezo huo.

Ushindi huo umeifanya Azam kufikisha pointi 39 na katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara iko nyuma ya vinara, Yanga yenye pointi 45 ikifuatiwa na Simba yenye pointi 44.

Mabao yote mawili ya Azam katika mechi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam yalifungwa na Gibril Sillah.

**Taoussi aliliambia gazeti hili timu yake itaendelea kucheza kwa kupambana ili kuhakikisha inatimiza malengo yake ya kutwaa ubingwa msimu huu.**

Kocha huyo alisema anajivunia kiwango kizuri kilichoonyeshwa na wachezaji wake katika mchezo huo.

"Walionyesha ufundi, walicheza mechi huku wakifurahia, muhimu tumepata pointi tatu," aliongeza kocha huyo.

Naye Kocha Mkuu wa KMC, Kally Ongalla, alisema alikiandaa vyema kikosi chake kusaka ushindi lakini hawakuwa na bahati katika mchezo huo.

Kally alisema wachezaji wake walifanya makosa kipindi cha kwanza na wapinzani wao walitumia nafasi hiyo, lakini kipindi cha pili walibadilika na kutawala mchezo.

"Kuna mambo mazuri walionyesha, haikuwa siku yetu, na kuna vitu tutavifanyia kazi, kuna tatizo la uzoefu pia lilionekana lakini kwa namna tulivyocheza, tulistahili ushindi," alisema Kally, ambaye aliwahi kuwa mchezaji na kocha wa zamani wa Azam.

Kabla ya matokeo ya mechi ya jana kati ya Singida Black Stars dhidi ya Kagera Sugar, KenGold yenye pointi sita inaendelea kuburuza mkia.

Ligi Kuu Tanzania Bara itaendelea tena kesho kwa Pamba Jiji kuikaribisha Azam kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza huku Dodoma Jiji wakiifuata Namungo kwenye Uwanja wa Majaliwa ulioko Ruangwa mkoani, Lindi.



Beki wa Azam FC, Paschal Msindo (kulia), akiwania mpira dhidi ya mchezaji wa KMC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam. Azam ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

## Fadlu amkingia 'kifua' Chasambi

INATOKA UK. 24

hani tutafanya vizuri," Ahmed alisema.

Naye Kocha Mkuu wa Fountain Gate, Robert Matano, alisema alichofanya ni kufunga njia za kukimbia za wachezaji wa Simba.

"Simba wana njia zao za kukimbia, wanapenda kwenda pembeni na kutumia mabeki kupiga krosi, nikazuia hilo, mtaona leo (juzi), hakukuwa na krosi za hatari, pili kipindi cha pili nilifanya mabadiliko ya wachezaji watano kwa mpigo, wenye uwezo wa kuuchezea mpira ili tutawale kati na kusaka bao la kusawazisha, tukafanikiwa," alisema Matano, ambaye ni raia wa Kenya.

Matokeo ya mchezo huo yameifanya Simba kushindwa kupanda kileleni, sasa ikishika nafasi ya pili ikiwa na pointi 44 huku vinara Yanga wakitawala baada ya kujikusanyia pointi 45, wakati Fountain Gate imefikisha pointi 21, ikiwa nafasi ya sita kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Simba imesharejea Dar es Salaam tayari kujiandaa kuikaribisha Tanzania Prisons katika mechi ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa Jumanne kwenye Uwanja wa KMC Complex.

## Bingwa mpya Dar kupatikana leo Kinesi

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Bara inatarajia kukutana na Barberian katika mechi ya Fainali ya Ligi ya Soka Mkoa wa Dar es Salaam itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Kinesi, imethibitishwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kaimu Meneja Mashindano wa Chama cha Mpira wa Miguu Mkoa wa Dar es Salaam (DRFA), Kibunge Tito, alisema maandalizi yote kuelekea fainali hiyo yamekamilika.

Tito alisema DRFA inazipongeza timu zote zilizoshiriki ligi hiyo kuanzia ngazi ya wilaya kwa sababu ndio zimepelekea hatua ya fainali ya mkoa kufanyika leo.

Aliongeza chama hicho kinazipongeza timu zote zilizoshiriki ligi pamoja na viongozi wa wilaya kwa kusimamia vyema kanuni na taratibu zilizowekwa katika ligi zao.

"Tumefurahishwa sana na ushindani ambao ulionyeshwa na timu zote zilizokuwa zinashiriki msimu huu kuanzia ngazi ya wilaya, pia tunazipongeza wilaya zetu zote kwa kuendesha vyema ligi zake, hii imepelekea kupata wawakilishi bora.

DRFA inapenda kuwakaribisha wadau wote wa soka jijini na mikoa jirani kwa ajili ya kushuhudia bingwa mpya akipatikana, tunawaalika pia makocha wa timu mbalimbali kuhudhuria ili kushuhudia vipaji vitakavyoonyeshwa katika mchezo huo wa fainali," alisema Tito.

Mgeni rasmi katika mechi ya fainali anatarajiwa kuwa Mwenyekiti wa DRFA na Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Lameck Nyambaya.

# Michezo

Jumamosi Februari 8, 2025

Nipashe




Amorim aanika siri Rashford kuondoka UKURASA 21

# Fadlu amkingia 'kifua' Chasambi

## Kocha huyo aomba mchezaji wake 'asisakamwe' kwa sababu...

**Na Adam Fungamwango**

TUKUBALI matokeo, Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, amewaomba wanachama na mashabiki wa timu hiyo kuacha 'kumsakama' winga, Ladack Chasambi, na badala yake wanatakiwa kumjenga kufuatia kosa alilofanya katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Fountain Gate na kupelekea kugawana pointi.

Katika mchezo huo, Chasambi, alijifunga na kuipa Fountain Gate bao la kusawazisha baada ya kurudisha mpira uliomshinda kuokoa kipa, Moussa Camara, aliyekuwa mbali na lango na kujaa wavuni.

Bao hilo la dakika ya 57, limekuwa gumzo kubwa katika mitandao ya kijamii, mijadala ya redioni, televisheni na kwenye vijiwe vya soka, kila mmoja akiongea lake, lakini likionekana kuwakera wanachama na mashabiki wa Simba kwa madai hakukuwa na ulazima wa kurudisha nyuma mpira huo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Fadlu alisema huu ni wakati wa 'kumpa moyo' mchezaji huyo na kuwa nyuma yake katika kipindi hiki kigumu anachopitia, ili kuokoa kipaji chake.

Fadlu alisema kufanya makosa ni sehemu ya mchezo wa mpira wa miguu na anaamini mambo yatakwenda vyema katika mechi zinazofuata.

"Tumehuzunika, tumetengeneza nafasi nyingi lakini tumeshindwa kuzitumia, yote si muhimu ila jambo la muhimu zaidi ni kumtetea Ladack Chasambi. Amejifunga, kutakuwa na maneno mengi, lakini tuangalie ni mchezaji chipukizi, ana kipaji ambacho kinaweza kuisaidia nchi siku za usoni, hili alilopitia ni somo kubwa kwake, atajifunza kupitia hili, tufanye kila njia kumtetea ili kutompoteza kwa sababu atashindwa tena kucheza kwa kujiamini," alisema Fadlu.

Kocha huyo aliongeza anadhani haikuwa siku yao kuvuna pointi tatu, kwa sababu walifanya kila kitu sahihi, lakini walikosa mabao mengi.

"Nadhani haikuwa siku yetu kwa sababu hata baada ya Chasambi kufanya makosa, tumekosa mabao ya wazi, kuna nafasi ya mwisho tuliikosa ya Ateba (Leonel) na Steven Mukwala waligongana wenyewe, kama usipofunga nafasi kama ile, haustahili kushinda maana huenda siyo siku yako," Fadlu alisema.

Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema walipata matokeo ambayo hakuna Mwana-Simba aliyetarajia.

Ahmed alisema hawakutoka sare kutokana na ubora wa wapinzani wao na wao hawakuwa katika ubora ule uliozoeleka.

"Ni matokeo mabaya tuliyoyapata, hakuna Mwana-Simba aliyetarajia, baada ya matokeo mazuri mfululizo, kila mmoja alitegemea Simba itashinda mchezo huu.

Hatukutoa sare kwa sababu ya ubora wa wapinzani wetu, ila tumejidhuru sisi wenyewe, tunawapa pole wanachama na mashabiki wote wa Simba, nasema tuna michezo 13 iliyobakia, nad-

INAENDELEA UK. 23



Chasambi

## Yanga, Coastal kukutana FA

**Faustine Feliciane na Adam Fungamwango**

WAKATI Yanga ikipangwa kukutana na Coastal Union ya Tanga katika mechi ya hatua ya 32 Bora ya mashindano ya Kombe la FA, mabingwa hao watetezi wamesema bado wana imani na straika wao, Prince Dube, licha ya nyota huyo kupoteza nafasi nyingi za kufunga mabao kwenye michezo mbalimbali anayocheza.

Katika droo ya mashindano ya FA iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana inaonyesha mshindi wa mechi hiyo atakutana na mshindi wa mchezo mwingine kati ya Polisi Tanzania au Songea United ya mkoani Ruvuma, zote zinashiriki Ligi ya Championship.

Simba yenyewe imepangwa kukutana na TMA Stars na mshindi atakutana na kati ya 'Maafande' wa Tanzania Prisons au Bigman FC huku Azam FC itamenyana na Mbeya City wakati Singida Black Stars itakutana na Leo Tena na Transit Camp itawafuata Tabora United kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani Tabora.



Mechi nyingine za hatua hiyo Mashujaa watacheza dhidi ya Geita Gold, Kagera Sugar watawakaribisha Namungo na vinara wa Ligi ya Championship watawaalika Towns Stars.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema jana anashangaa kuona kukosa mabao kwa Dube imekuwa 'mjadala mkubwa' kuliko magoli anayofunga Mzimbabwe huyo.

Kamwe alisema katika mchezo uliopita dhidi ya KenGold, straika huyo alifunga mabao mawili na kutoa pasi moja ya bao, lakini hilo halijadiliwi, badala yake amekuwa akihukumiwa kwa zile nafasi alizokosa.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >